**SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR**

**WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI**

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**ILIYOWASILISHWA NA**

**MHESHIMIWA DKT. KHALID SALUM MOHAMED (MBM)**

**KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MEI, 2023**

## VIONGOZI WA WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI - ZANZIBAR



**Mhe. Dk. Khalid Salum Mohamed (MBM)**
***Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi***
***Zanzibar***



**Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Alwardy**
***Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi***
***Zanzibar***



**Nd. Khadija Khamis Rajab**
***Katibu Mkuu***
***WUMU***
***Zanzibar***



**Nd. Shomari Omar Shomari**
**Naibu *Katibu Mkuu***
***WUMU***
***Zanzibar***



**Nd. Ibrahim Saleh Juma**
**Afisa Mdhamini**
***WUMU Pemba***

## YALIYOMO


**YALIYOMO**............................................................................i

**ORODHA YA VIAMBATANISHO**..........................................................iii

**A. UTANGULIZI** ..........................................................................1

**B. MAJUKUMU NA MUUNDO WA WIZARA** ..........................................3

**C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI, 2022 HADI MACHI, 2023**..................................................4

C.1. Ukusanyaji wa Mapato kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 ..........................................................................4
C.2. Fedha zilizopatikana kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 ..........................................................................4
C.3. Utekelezaji wa Programu za Wizara kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023..........................................................................5

**C.3.1. PROGRAMU YA USAFIRISHAJI** ..................................5
C.3.1.1. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji ..................................................5

**C.3.2. PROGRAMU YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA)** ..........................................................23
C.3.2.1. Programu Ndogo ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA..24

**C.3.3. PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA** ..........................................................29
C.3.3.1. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji.. ....................................................................30
C.3.3.2. Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara..........................................................................31
C.3.3.3. Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba.. ........................................................................ 34

**D.UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA KWA KIPINDI CHA JULAI 2022 HADI MACHI 2023 PAMOJA NA MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024**...............................35

D.1 SHIRIKA LA BANDARI ZANZIBAR..................................................35
D.2 SHIRIKA LA MELI ZANZIBAR.........................................................42
D.3 MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI ZANZIBAR.................................45
D.4 MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR............................51
D.5 MAMLAKA YA USAFIRI NA USALAMA BARABARANI........................57
D.6 WAKALA WA MIUNDOMBINU YA TEHAMA ....................................58

**E.MUELEKEO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI KWA KILA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024** ..........60

E.1. VIPAUMBELE VIKUU VYA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 ..........60
E.2. MUHTASARI WA MAELEZO KWA KILA PROGRAMU NA MALENGO YANAYOTARAJIWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 .......... 61

**E.2.1 PROGRAMU YA USAFIRISHAJI.......... 61**
E.2.1.1 Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji .......... 62

**E.2.2 PROGRAMU YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA) .......... 65**
E.2.2.1 Programu Ndogo ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA ..........65

**E.2.3 PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA ..........66**
E.2.3.1 Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji.67
E.2.3.2 Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara ..........68
E.2.3.3 Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba ..........69

**F. HITIMISHO**..........70

**G. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2023/2024** ..........72

## ORODHA YA VIAMBATANISHO


Kiambatanisho Nambari 1: Makusanyo ya Mapato ya Wizara Unguja na Pemba................................74

Kiambatanisho Nambari 2A . Fedha zilizopatikana kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023...............74

Kiambatanisho Nambari 2B: Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa kila programu kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 ..................................................75

Kiambatanisho Nambari 3A: Ukaguzi wa Vyombo vya Moto kwa Julai 2022 hadi Machi 202384.............76

Kiambatanisho Nambari 3B: Ruhusa za Njia na Usafirishaji Julai 2022 hadi Mach 2023...........................76

Kiambatanisho Nambari 3C: Beji za Utingo na Madereva zilizotolewa kwa Kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023.........................76

Kiambatanisho Nambari 4: Idadi ya vyombo vya moto vilivyofanyiwa matengenezo Unguja na Pemba Julai, 2022 hadi Machi, 2023....................................................76

Kiambatanisho Nambari 5A: Orodha ya Barabara zilizofanyiwa usafi wa ukataji majani, Usafishaji misingi na makalvati Unguja na Pemba............................................77

Kiambatanisho Nambari 5B: Orodha ya Barabara zilizofanyiwa matengenezo ya kawaida ya uzibaji mashimo..............................80

Kiambatanisho Nambari 6: Orodha ya Barabara za Mjini km 100.9 zinazoendelea kujengwa........81

Kiambatanisho Nambari 7: Orodha ya Barabara za Ndani km 275.9 zinazoendelea kujengwa Unguja na Pemba .... ............83

| | |
|---|---|
| Kiambatanisho Nambari 8: | Orodha ya Minara 42 ya Mawasiliano iliyojengwa Unguja na Pemba Julai, 2022 hadi Machi, 2023.................86 |
| Kiambatanisho Nambari 9A: | Orodha ya Taasisi zilizoungaishwa na Mkonga wa Mawasiliano Julai, 2022 hadi Machi,2023..................................88 |
| Kiambatanisho Nambari 9B: | Idadi ya Mifumo na Majina ya Taasisi zilizohifadhi Mifumo katika kituo cha kuhifadhia taarifa..................................90 |
| Kiambatanisho Nambari 10A: | Wafanyakazi waliopatiwa mafunzo ya Muda Mrefu kwa mwaka 2022/2023.....90 |
| Kiambatanisho Nambari 10B: | Wafanyakazi waliopatiwa mafunzo ya Muda Mfupi kwa mwaka wa fedha 2022/2023......................................... 91 |
| Kiambatanisho Nambari 11: | Meli za Kigeni zilizopatiwa huduma za Uwakala kwa Julai, 2022 hadi Machi, 2023....................................................91 |
| Kiambatanisho Nambari 12A: | Idadi ya Ndege zilizohudumiwa kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023....................................................91 |
| Kiambatanisho Nambari 12B: | Kampuni za Ndege zilizotumia Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume kwa Mwaka 2022/2023...........92 |
| Kiambatanisho Nambari 12C: | Idadi ya Abiria waliohudumiwa kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023....................................................93 |

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ili liweze kupokea, kuzingatia, kujadili na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa kazi za kawaida na kazi za Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

2. **Mheshimiwa Spika,** nianze kwa kumshukuru Allah (S.W) kwa kutujaalia uhai na afya njema na kutuwezesha kuhudhuria katika kikao hiki cha Baraza la Wawakilishi kinachojadili Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ikiwa leo hii tunajadili utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na mwelekeo wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

3. **Mheshimiwa Spika,** kwa dhati kabisa nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuniamini kuiongoza Wizara hii. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa Maelekezo na Miongozo anayoitoa kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi katika kuendeleza sekta za Ujenzi wa Miundombinu ya Usafiri, Usafirishaji na Mawasiliano. Maelekezo na miongozo anayoitoa Mheshimiwa Rais inatusaidia sana kuongeza ufanisi wa kazi na kasi ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii. Pia, nampongeza Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa kuimarisha maslahi ya Watumishi wa Serikali kwa kuwaongezea mishahara iliyopelekea kuongeza ari ya uwajibikaji na hatimae kuleta ufanisi katika kazi. Vilevile, nampongeza Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa umahiri wake mkubwa katika kuendelea kuiongoza vyema Zanzibar na kuwaletea maendeleo wananchi wake. Kwa hakika chini ya Uongozi wake, Serikali

ya Mapinduzi ya Zanzibar imetekeleza kwa vitendo ahadi alizozitoa kwa wananchi wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025. Kipekee kabisa, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuiongoza vyema Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa lengo la kuleta maridhiano na kuwaunganisha Wazanzibari wote na kuhakikisha amani, utulivu na mshikamano unaendelea kudumu katika nchi yetu.

4. **Mheshimiwa Spika,** Pia nawapongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa namna ambavyo wamekuwa wakimsaidia Mheshimiwa Rais katika kusimamia na kuongoza shughuli zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Nawashukuru viongozi wetu hawa kwa miongozo wanayotupatia katika Wizara hii ambayo imetuwezesha kutekeleza majukumu kwa ufanisi, uwazi na umakini. Aidha, naomba kumpongeza tena kwa dhati Makamo wa Pili wa Rais Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, kwa kuongoza na kusimamia vyema shughuli za Serikali pamoja na kuratibu vizuri shughuli zote za Baraza lako Tukufu.

5. **Mheshimiwa Spika,** napenda pia nikupongeze wewe binafsi kwa umahiri, hekima na busara unazozitumia katika kuliongoza Baraza la Wawakilishi ambalo ni muhimili muhimu wa kupitisha maamuzi kwa manufaa ya nchi yetu. Maamuzi hayo yamethibitisha uwezo wa Baraza hili katika kusimamia demokrasia na utawala bora nchini mwetu. Aidha, pongezi pia nazitoa kwa Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kukusaidia kuendesha shughuli za Baraza hili.

6. **Mheshimiwa Spika,** kwa mapenzi makubwa sana natoa shukurani zangu kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati chini ya uongozi makini wa Mwenyekiti wake Mheshimiwa Yahya Rashid Abdalla, Mwakilishi wa kuchaguliwa na Wananchi katika Jimbo la Kwahani kwa maoni, hoja, mapendekezo, ushauri na maelekezo ambayo yanaisaidia sana Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi katika utekelezaji wa majukumu yake. Kamati hii ilipata nafasi ya kutembelea Taasisi na miradi mbalimbali iliyomo ndani ya Wizara hii na kutoa ushauri na maoni yenye lengo la kuimarisha utekelezaji wa miradi hiyo. Ushauri, maoni na maelekezo hayo, yataendelea kuzingatiwa kwa vitendo wakati wa utekelezaji wa bajeti hii.

## B. MAJUKUMU NA MUUNDO WA WIZARA

7. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ina jukumu la kusimamia sekta ya Usafirishaji na Mawasiliano. Wizara inatekeleza majukumu hayo kupitia idara tatu (3) na Taasisi nane (8) zinazojitegemea zinazounda Wizara hii ambazo; ni Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Mawasiliano pamoja na Ofisi Kuu Pemba ambayo inaratibu Shughuli za Wizara kwa upande wa Pemba. Kwa Taasisi zinazojitegemea ni; Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Zanzibar, Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, Shirika la Bandari Zanzibar, Shirika la Meli Zanzibar, Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar, Wakala wa Barabara Zanzibar pamoja na Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar.

## C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI, 2022 – MACHI, 2023

### C.1. Ukusanyaji wa Mapato kwa Kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023

8. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ilikadiria kukusanya jumla ya TSH 7,028,974,000. Kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 ilikadiria kukusanya jumla ya TSH 5,177,446,495. Hadi kufikia Machi, 2023, jumla ya TSH 4,070,212,937 zimekusanywa sawa na asilimia 78.6 ya makadirio ya robo tatu na asilimia 57.9 kwa makadirio ya mwaka. **Kiambatanisho nambari 1** kinahusika.

### C.2. Fedha Zilizopatikana kwa Kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023

9. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kupitia Programu zake kuu tatu (3) kwa mwaka wa fedha 2022/2023, iliidhinishiwa na Baraza la Wawakilishi kutumia jumla ya TSH 581,458,878,692 kati ya fedha hizo TSH 10,587,671,546 ni mshahara, TSH 6,864,207,146 kwa kazi za kawaida na TSH 564,007,000,000 kwa kazi za maendeleo. Kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Wizara ilipanga kutumia jumla ya TSH 420,635,237,922. Kati ya fedha hizo TSH 6,022,190,652 kwa kazi za kawaida, TSH 7,758,047,270 mshahara na TSH 406,855,000,000 kwa kazi za maendeleo.

Hadi kufikia Machi, 2023, jumla ya TSH 84,283,504,932 zimepatikana sawa na asilimia 20 ya makadirio ya bajeti kwa kipindi cha robo tatu na asilimia 14.4 kwa makadirio ya bajeti kwa mwaka. Kati ya fedha hizo, TSH 72,971,447,148 ni kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 39.4 ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 28 ya makadirio ya mwaka, TSH 7,758,047,270 ni mshahara sawa na asilimia 100 ya

makadirio ya miezi tisa na asilimia 73 kwa mwaka na TSH 3,554,010,514 sawa na asilimia 59 ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 52 ya makadirio ya mwaka kwa kazi za kawaida na ruzuku. **Kiambatanisho nambari 2A na 2B** kinatoa ufafanuzi.

### C.3. Utekelezaji wa Programu za Wizara kwa Kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023

10. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kutekeleza Bajeti kwa kutumia Mfumo wa Programu (PBB). Hivyo, taarifa ya utekelezaji wa programu za Wizara ninayoiwasilisha imezingatia Programu ambazo tuliziwasilisha katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023 na kuidhinishwa na Baraza lako Tukufu. Hivyo, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi inatekeleza kazi zake kupitia Programu kuu tatu (3) na Programu ndogo tano (5) kama ifuatavyo: -

### C.3.1. PROGRAMU YA USAFIRISHAJI

11. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ina lengo la kuimarisha miundombinu na huduma za usafiri ili ziwe bora, salama na endelevu. Matokeo yanayotarajiwa kupatikana ni kuwepo kwa miundombinu na huduma bora zenye usalama za usafiri. Programu ya Usafirishaji ina Programu ndogo moja (1) ambayo ni Programu ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji.

#### C.3.1.1. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji.

12. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Idara moja (1) na Taasisi tatu (3) zinazojitegemea ambazo ni Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Zanzibar, Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar na Wakala wa Barabara Zanzibar. Wizara kupitia programu hii imetekeleza mambo yafuatayo:-

## 1. MAMLAKA YA USAFIRI NA USALAMA BARABARANI ZANZIBAR

13. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kupitia programu ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji ina jukumu la kusimamia usafiri barabarani kwa kudhibiti usalama wa watumiaji wa barabara, utoaji wa huduma za usafiri barabarani pamoja na kusimamia Kamati ya Kitaifa ya Usalama Barabarani. Aidha, katika kutekeleza majukumu hayo, Mamlaka inafanya shughuli za ukaguzi wa vyombo vya moto pamoja na kutoa leseni za njia kwa vyombo hivyo (Licenses), kutoa leseni kwa vyuo vya udereva na walimu wao, kutoa leseni za madereva wanafunzi (learners), kuwafanyia majaribio ya nadharia na vitendo madereva wanafunzi, kutoa ruhusa za njia na usafirishaji wa abiria na mizigo, kutoa beji za utingo na madereva pamoja na kutoa vibali kwa madereva wa kigeni wanaotaka kuendesha vyombo vya moto hapa Zanzibar.

14. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kupitia Programu ya Usimamizi wa Miuondombinu na Huduma za Usafirishaji imetekeleza kazi zifuatazo:-

a. **Ukaguzi wa Vyombo vya Moto:** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilipanga kufanya ukaguzi wa vyombo vya moto 64,796 Unguja na Pemba, na kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 ilipanga kufanya ukaguzi wa vyombo vya moto 48, 607. Hadi kufikia Machi 2023 Mamlaka imekagua jumla ya vyombo vya moto 47,225 Unguja na Pemba ili kuhakikisha kuwa vipo katika hali ya uzima na usalama ambavyo ni sawa na asilimia 97 ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 73 ya makadirio ya mwaka. Kati ya vyombo hivyo, 41,087 vimekaguliwa Unguja na 6,138 vimekaguliwa Pemba. **Kiambatanisho nambari 3A** kinahusika.

b. **Utoaji wa Ruhusa za Njia na Usafirishaji:** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilipanga kutoa ruhusa za njia na usafirishaji 12,804, na kwa kipindi cha miezi tisa ilipanga kutoa ruhusa za njia na usafirishaji 9,618. Hadi kufikia Machi 2023, jumla ya ruhusa za njia na usafirishaji 12,509 kwa gari mbalimbali zinazotoa huduma za usafirishaji wa abiria na mizigo zimetolewa Unguja na Pemba sawa na asilimia 130 ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 98 ya makadirio ya mwaka. Kati ya ruhusa hizo, 11,190 zimetolewa Unguja na ruhusa 1,319 zimetolewa Pemba. **Kiambatanisho nambari 3B** kinahusika.

c. **Utoaji wa Leseni kwa Gari za Biashara:** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilipanga kutoa leseni 14,222 kwa gari za biashara, na kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 imepanga kutoa leseni 10,606 kwa Unguja na Pemba. Hadi kufikia Machi 2023 jumla ya leseni 10,054 zimetolewa kwa gari za biashara aina mbalimbali zinazotoa huduma ya usafirishaji wa abiria na mizigo sawa na asilimia 95 ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 71 ya makadirio ya mwaka. Kati ya leseni hizo, leseni 8,606 zimetolewa Unguja na leseni 1,092 zimetolewa Pemba.

d. **Majaribio ya Madereva:** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilipanga kuwafanyia majaribio ya nadharia na vitendo jumla ya madereva 11,365, na kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 ilipanga kuwafanyia majaribio madereva 8,531 Unguja na Pemba. Hadi kufikia Machi 2023, Mamlaka imefanikiwa kuwafanyia majaribio ya nadharia na vitendo jumla ya madereva 7,531 sawa na asilimia 88 ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 75 ya makadirio ya mwaka. Ikiwa madereva 6,679 wamefanyiwa majaribio Unguja na madereva 852 wamefanyiwa majaribio Pemba.

**e. Utoaji wa Beji za Utingo na Madereva:** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilipanga kutoa beji za utingo na madereva wa vyombo vya biashara aina mbalimbali 9,834, na kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 ilipanga kutoa beji za utingo na madereva wa vyombo vya moto 7,256 Unguja na Pemba. Hadi kufikia Machi 2023, jumla ya beji 7,575 zimetolewa kwa utingo na madereva wa vyombo vya biashara Unguja na Pemba sawa na asilimia 104 ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 77 ya makadirio ya mwaka. Kati ya beji hizo, 6,936 zimetolewa Unguja na 639 zimetolewa Pemba. Kiambatanisho namba 3C kinahusika.

**f. Utoaji wa Leseni za Madereva Wanafunzi:** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilipanga kutoa leseni za kujifundishia vyombo vya moto kwa madereva wanafunzi 15,005 na kwa kipindi cha miezi tisa (Julai, 2022 hadi Machi, 2023) ilipanga kutoa leseni 11,250. Hadi kufikia Machi 2023 jumla ya leseni za madereva wanafunzi 15,789 zimetolewa Unguja na Pemba sawa na asilimia 140 ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 105 ya makadirio ya mwaka. Kati ya leseni hizo, 14,441 zimetolewa Unguja na 1,348 zimetolewa Pemba.

**g. Utoaji wa Vibali kwa Madereva Wageni:** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilipanga kutoa vibali 20,000 vya ruhusa ya kuendesha vyombo vya moto kwa madereva wageni, na kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 ilipanga kutoa vibali 16,057 Unguja na Pemba. Hadi kufikia Machi 2023 jumla ya vibali 19,280 vimetolewa kwa Unguja na Pemba sawa na asilimia 120 ya makadirio ya miezi tisa na asilimi 96 ya makadirio ya mwaka. Kati ya vibali hivyo 19,243 vimetolewa Unguja na 37 vimetolewa Pemba.

**h. Kuanzisha Mfumo wa Adhabu za Papo kwa Papo Barabarani**
Katika kuhakikisha ajali za barabarani zinazosababishwa na madereva wazembe na wasiotii sheria za usalama barabarani zinapunguwa, Wizara imeanzisha mfumo wa adhabu za Papo kwa Papo barabarani ambapo kwa sasa madereva wazembe na wasiotii sheria hizo huadhibiwa kwa kutozwa faini za papo kwa papo pindi wanapobainika kuwa wametenda makosa yanayohusiana na uvunjaji wa sheria hizo za usalama barabarani. Jumla ya makosa 4,910 yameripotiwa kwa kipindi cha mwezi wa Machi na Aprili, 2023 na kutozwa faini.

**Mapato na Matumizi**

15. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani ilikadiria kukusanya jumla ya TSH 3,924,974,000 Unguja na Pemba. Kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, ilikadiria kukusanya jumla ya TSH 2,925,734,000 na hadi kufikia Machi, 2023, jumla ya TSH 2,876,065,313 zimekusanywa sawa na asilimia 98 ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 73 ya makadirio ya mwaka.

16. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani ilipangiwa kutumia jumla ya TSH 2,012,627,681 Unguja na Pemba ikiwa TSH 854,500,000 ni Ruzuku kwa kazi za kawaida na TSH 729,100,000 ni ruzuku ya mshahara. Hadi kufikia Machi, 2023, jumla ya TSH 1,155,957,692 zimetumika kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na mshahara sawa na asilimia 57.4 ya makadirio ya bajeti. Kati ya fedha hizo, mshahara ni TSH 864,267,692 na TSH 291,690,000 ni matumizi mengineyo.

## 2. WAKALA WA KARAKANA KUU YA MAGARI ZANZIBAR

17. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Karakana Kuu ya Magari kupitia programu ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji imepewa jukumu la kuvifanyia matengenezo vyombo vya moto vya Serikali na binafsi kupitia Karakana zake zilizopo Unguja na Pemba pamoja na kutoa ushauri wa ununuzi na uuzaji wa gari za Serikali.

18. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kupitia Wakala wa Karakana Kuu ya Magari imefanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo; -

    a. **Matengenezo ya Vyombo vya Moto (Magari) vya Serikali na Binafsi:** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wakala wa Karakana Kuu ya Magari ilipanga kufanya matengenezo ya vyombo vya moto 1,200 vya Serikali na Binafsi kwa Unguja na Pemba. Kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Wakala ilipanga kufanya matengenezo ya gari 900. Hadi kufikia Machi 2023 jumla ya vyombo vya moto 1,396 zimefanyiwa matengenezo Unguja na Pemba sawa na asilimia 155 ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 116 ya makadirio ya mwaka. Kati ya gari hizo, 1,088 ni za Serikali na 308 ni gari za watu binafsi. Aidha, jumla ya gari 1,256 zimefanyiwa matengenezo Unguja na gari 140 zimefanyiwa matengenezo Pemba. **Kiambatanisho Nambari 4** kinahusika.

    b. **Utoaji wa Ushauri wa Kitaalamu Juu ya Ununuzi na Uuzaji wa Vyombo vya Moto vya Serikali:** Wakala wa Karakana Kuu ya Magari kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 ilipanga kutoa ushauri wa Kitaalamu wa ununuzi wa vyombo vya moto vya Serikali kwa Taasisi 15 na kufanikiwa kutoa ushauri kwa Taasisi 11 za Serikali katika ununuzi wa vyombo hivyo sawa na asilimia 73 ya makadirio

ya miezi tisa. Taasisi hizo ni:- Tume ya Ukimwi Zanzibar; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; Kamisheni ya Utalii Zanzibar; Shirika la Umeme Zanzibar; Ofisi ya Rais Fedha na Mipango; Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji; Kamisheni ya Ardhi; Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kusini Unguja; Zimamoto na Uokozi; Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali na Wizara ya Maji, Nishati na Madini Zanzibar.

**c) Uimarishaji wa Karakana Unguja na Pemba:** Wakala inaendelea kuziimarisha Karakana zake zilizopo Unguja na Pemba kwa kuzifanyia matengenezo mashine mbali mbali za kutolea huduma za matengenezo ya magari pamoja na kufanya matengenezo sehemu ya kufanyia matengenezo ya magari. Pia, Wakala imefanikiwa kuandaa Mpango Mkakati (Strategic Plan) wa miaka mitatu 2023/2026, Mpango wa Kibiashara (Business Plan) wa Karakana kwa kipindi cha miaka mitano 2023/2028 pamoja na kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi 7 na ya muda mfupi wafanyakazi 11 katika fani tofauti ikiwa ni hatua za kuimarisha huduma za karakana kwa Serikali na Wananchi kwa ujumla Unguja na Pemba.

**Mapato na Matumizi**

**19.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wakala wa Karakana kuu ya magari ilikadiria kukusanya jumla ya TSH 100,000,000, na kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, ilikadiria kukusanya jumla ya TSH 75,000,000 na hadi kufikia Machi, 2023, jumla ya TSH 52,430,618 zimekusanywa sawa na asilimia 69.9 ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 52.43 ya makadirio ya mwaka.

**20.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wakala wa Karakana Kuu ya Magari

ilipangiwa kutumia jumla ya TSH 1,513,685,745 ikiwa ni ruzuku kwa kazi za kawaida na Mshahara. Hadi kufikia Machi, 2023 jumla ya TSH 1,119,039,178 zimetumika kazi za kawaida sawa na asilimia 73.9 ya makadirio ya bajeti. Kati ya fedha hizo, TSH 793,496,178 ni Mshahara na TSH 325,543,000 ni Ruzuku kwa matumizi ya mengineyo.

## 3. WAKALA WA BARABARA ZANZIBAR

21. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Barabara Zanzibar kupitia Programu ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji ina jukumu la kujenga, kutunza na kuzifanyia matengenezo barabara mbalimbali za Unguja na Pemba ili ziweze kupitika kwa usalama muda wote kwa lengo la kurahisisha shughuli za kiuchumi na kijamii ziweze kufanyika kwa ufanisi mkubwa.

22. **Mheshimiwa Spika,** Kazi za utunzaji na matengenezo ya barabara Unguja na Pemba zinagharamiwa na Mfuko wa Barabara Zanzibar. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Wakala wa Barabara Zanzibar imefanikiwa kuzifanyia matengenezo barabara za Unguja na Pemba kama ifuatavyo: -

### a. Barabara ya Garagara hadi Mtoni Kidatu km 3

23. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 kazi ilizofanyika ni uwekaji kifusi tabaka la mwisho kwa urefu wa kilomita 1.5. Ujenzi wa barabara hii umefikia asilimia 60 ya utekelezaji na kazi za ujenzi zinaendelea. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 394,339,000 na hadi kufikia machi, 2023 jumla TSH 376,746,560 zimepatikana sawa na asilimia 95 ya makadirio.

**b. Ujenzi wa Msingi wa Maji ya Mvua Eneo la Mfenesini Unguja**

24. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Barabara imekamilisha kwa asilimia 100 ujenzi wa msingi wa maji ya mvua wenye urefu wa mita 450 katika eneo la Mfenesini. Kazi za ujenzi zimefanywa na Kampuni ya Lukolo kutoka Dar es Salam chini ya usimamizi wa Wakala wa Barabara Zanzibar. Kazi hii ilichukua muda wa miezi mitatu na ilianza rasmi mwezi wa Januari, 2023. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, ujenzi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 1,305,628,350 na hadi kufikia Machi, 2023 jumla ya TSH 1,240,346,932 zimepatikana sawa na asilimia 95 ya makadirio.

**c. Matengenezo ya Barabara ya Jumbi - Tunguu km 4.5**

25. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Barabara Zanzibar ilipanga kuifanyia matengenezo barabara ya Jumbi - Tunguu yenye urefu wa kilomita 4.5 kwa kiwango cha lami. Kazi za usanifu na michoro zimefanyika pamoja na kuanza kwa shughuli za usafishaji wa barabara hiyo kwa kuondoa miti pembezoni mwa barabara. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 1,879,000,000 na hadi kufikia Machi 2023 hakuna fedha zilizopatikana.

**d. Barabara ya Uzini kwa Sheha – Msikiti wa Ijumaa km 1.2 kwa Kiwango cha Lami**

26. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wakala wa Barabara ilipanga kuifanyia matengenezo barabara ya Uzini kwa sheha hadi Msikiti wa Ijumaa yenye urefu wa kilomita 1.2 kwa kiwango cha lami. Hadi kufikia Machi 2023 kazi ziliyofanyika ni usanifu wa barabara ikiwa ni sehemu ya matayarisho ya ujenzi. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, ujenzi wa barabara hii ulipangwa kutumia jumla ya TSH. 395,440,000 na hadi kufikia Machi, 2023 hakuna fedha iliyopatikana.

**e. Barabara ya Kipapo – Mgelema- Wambaa km 9.3 kwa Kiwango cha Lami**

**27. Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Barabara ilipaga kuijenga barabara ya Kipapo-Mgelema - Wambaa yenye urefu wa km 9.3 kwa kiwango cha lami. Hadi kufikia Machi 2023 jumla ya kilomita 8.5 zimewekwa kifusi tabaka tofauti na jumla ya km 5.6 zimeshawekwa lami ya maji ikiwa ni matayarisho ya uwekaji wa lami ngumu na kazi za ujenzi zinaendelea na zimefikia asilimia 61. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 1,545,230,000 na hadi kufikia Machi, 2023 jumla ya TSH 400,000,000 zimepatikana sawa na asilimia 26 ya makadirio.

**f. Matengenezo ya Sehemu Korofi (Spot Improvement) kwa Maeneo ya Barabara za Unguja na Pemba kwa Kiwango cha Lami**

**28. Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Barabara kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilipanga kuzifanyia matengenezo barabara katika maeneo tofauti Unguja na Pemba zenye jumla ya mita za mraba 8,665 ili ziweze kupitika muda wote. Hadi kufikia Machi 2023, kazi za matengenezo ya barabara zilizofanyika ni uwekaji wa lami katika maeneo ya barabara ya Bububu Mshelishelini mita za mraba 595, Bububu silver sand mita za mraba 553, Bububu Skuli mita za mraba 1,120, Magomeni Jitini mita za mraba 650, Ujenzi wa eneo la maegesho Darajani Souk mita za mraba 4,615, Maegesho ya Msikiti Forodhani mita za mraba 935 na eneo la Ikulu mita za mraba 198. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wakala wa barabara ilipanga kutumia Jumla ya TSH 344,725,750 kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Unguja na Pemba na hadi kufikia machi, 2023 hakuna fedha iliyopatikana.

### g. Uimarishaji wa Usalama Barabarani kwa Unguja na Pemba

29. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Wakala wa Barabara Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilipanga kuweka alama na michoro ya usalama barabarani katika maeneo tofauti Unguja na Pemba. Hadi kufikia Machi 2023, maeneo ya barabara yaliyowekwa alama na michoro ya usalama barabarani ni Skuli ya Msingi Upenja, Binguni, Kianga, Salim Turkey na Pangeni na Skuli za Sekondari ya Benbella. Aidha maeneo mengine ni pamoja na Bububu, Kitope, eneo la Madrasa Kianga na barabara ya Kwamchina mwanzo. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, jumla ya TSH 80,000,000 zilitengwa kwa ajili ya kuweka alama za usalama barabarani Unguja na Pemba na hadi kufikia Machi 2023 hakuna fedha iliyopatikana katika kipindi hicho.

### h. Matengenezo ya Kawaida ya Barabara

30. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wakala wa Barabara ilipanga kuzifanyia matengenezo ya kawaida (Routine Maintenance) barabara zenye urefu wa kilomita 1,331 Unguja na Pemba, na kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, ilipanga kuzifanyia matengenezo ya kawaida barabara zenye urefu wa kilomita 1,010. Hadi kufikia Machi 2023, jumla ya kilomita 486.07 Unguja na Pemba zimefanyiwa usafi (ukataji wa majani pembezoni mwa barabara, usafishaji wa misingi ya maji na makalvati) sawa na asilimia 48 ya makadirio ya robo tatu. Kwa upande wa Unguja barabara zilizofanyiwa usafi ni kilomita 186.5 na Pemba kilomita 299.5. Aidha, kwa mwaka wa Fedha 2022/2023 Wakala wa barabara ilipanga kuziba mashimo jumla ya mita za mraba 12,000 Unguja na Pemba, na kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 ilipanga kuziba mashimo mita za mraba 9,690 na hadi kufikia machi, 2023

jumla ya mita za mraba 4455.8 zimezibwa mashimo sawa na asilimia 46 ya makadirio ya robo tatu. **Kiambatanisho nambari 5A na 5B** kinahusika.

Kwa mwaka wa fedha, 2022/2023, jumla ya TSH 900,000,000 zilitengwa na hadi kufikia Machi 2023 jumla ya TSH 242,416,050 zimepatikana sawa na asilimia 27 ya makadirio ya mwaka.

**i. Uendeshaji wa Shughuli za Ofisi**

**31. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wakala wa Barabara ilipanga kuendelea kuimarisha shughuli za kiutawala na kiutumishi pamoja na kuwajengea uwezo wafanyakazi 9 kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu. Hadi kufikia Machi, 2023 Wakala imefanikiwa kuimarisha shughuli za kiutumishi na Uendeshaji wa ofisi kwa kununua vifaa mbali mbali vya ofisi, kusimamia maslahi ya watumishi pamoja na kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi 13 na mafunzo ya muda mrefu Mfanyakazi mmoja. Aidha, jumla ya Wafanyakazi 535 walipatiwa mafunzo kuhusiana na maadili ya utumishi yaliyotolewa na Afisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala bora.

**Matumizi kwa Mwaka wa fedha 2022/2023.**

**32. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wakala wa Barabara Zanzibar ilipangiwa kutumia jumla ya TSH 5,470,650,888 ikiwa TSH 808,700,000 kwa kazi za kawaida na TSH 4,661,950,888 mshahara. Hadi kufikia Machi, 2023, jumla ya TSH 3,722,736,745 zimetumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 68 ya makadirio ya bajeti. Kati fedha hizo, TSH 3,527,448,445 ni mshahara na TSH. 195,288,300 ni ruzuku kwa matumizi mengineyo.

33. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Mfuko wa Barabara Zanzibar, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ilipangiwa kutumia jumla ya TSH 20,033,644,000 na hadi kufikia Machi, 2023, jumla ya TSH 2,519,959,914.5 zimepatikana sawa na asilimia 12.6 ya makadirio ya bajeti kwa ajili ya matengenezo ya barabara mbalimbali Unguja na Pemba.

## 4. IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

34. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia Programu ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji ina jukumu la kuratibu na kusimamia miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ilipanga kusimamia na kuratibu utekelezaji wa miradi ifuatayo:-

## MIRADI YA UIMARISHAJI WA USAFIRI WA BARABARA

### a. Barabara za Mjini Unguja Zenye Urefu wa Kilomita 100.9

35. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeanza kutekeleza mradi wa ujenzi wa barabara za Mjini zenye urefu wa kilomita 100.9 pamoja na ujenzi wa barabara za juu (Fly over) katika eneo la Amani na Mwanakwerekwe Round About. Mradi huu utahusisha ujenzi wa njia za waenda kwa miguu, uwekaji wa taa za kuongozea gari, taa za barabarani pamoja na misingi ya maji. Kazi za ujenzi zinatekelezwa na Kampuni ya CCECC kutoka China ambayo ilisaini Mkataba wa ujenzi tarehe 6 Agosti, 2022 kwa gharama ya fedha za Kimarekani USD 116,131,442.96. Mradi huu umeanza rasmi tarehe 1 Disemba, 2022 na unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 36. Fedha za mradi huu zinatolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

36. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 jumla ya km 4.5 za barabara ya Chukwani – Buyu km 2.7 na Msumbiji – kinyang'unya – Mwanakwerekwe km 1.8 zinaendelea kuwekwa kifusi na kuanza hatua za uwekaji wa lami. Orodha ya Barabara zinazotarajiwa kujengwa kupitia mradi huu zinaonekana katika **kiambatanisho nambari 6.**

37. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha, 2022/2023, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 135,600,000,000 kutoka Serikalini na hadi kufikia Machi, 2023, jumla ya TSH 40,488,929,656 zimepatikana sawa na asilimia 29.8 ikiwa ni malipo ya awali (Advance payment) kwa Mkandarasi.

**b. Barabara za Ndani Zenye Urefu wa Kilomita 275.9 Unguja na Pemba.**

38. **Mheshimiwa Spika.** Wizara inaendelea na ujenzi wa barabara za Ndani zenye urefu wa kilomita 275.9. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kazi za ujenzi zinatekelezwa na Kampuni ya IRIS/ASER kutoka Nchini Uturuki ambayo ilisaini Mkataba wa Ujenzi tarehe 22 Novemba, 2021 kwa gharama za USD Milioni 89.3 ikiwa ni gharama za ujenzi. Mradi huu ulianza rasmi tarehe 26 Machi, 2022 na unatarajiwa kukamilika ndani ya kipindi cha miezi 40. Aidha, ujenzi wa barabara hizi unasimamiwa na Wizara kupitia taasisi yake ya Wakala wa Barabara Zanzibar. Mradi huu umefikia asilimia 18 ya utekelezaji.

39. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, jumla ya km 21.4 zimekamilika kwa kiwango cha lami na jumla ya km 23.3 zimekamilika kwa kiwango cha kifusi. Orodha ya barabara zilizokamilika, zinazoendelea na ambazo bado ujenzi wake haujaanza zinaonekana katika **kiambatanisho Nambari 7.**

40. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa 2022/2023, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 30,000,000,000. Hadi kufikia Machi, 2023 jumla ya TSH 12,919,582,071 zimepatikana sawa na asilimia 43 ya makadirio ya bajeti.

**c. Barabara Kuu Nne (4) za Zanzibar km 130.6.**

41. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unajumuisha ujenzi wa barabara kuu za Unguja na Pemba zenye urefu wa kilomita 130.6 zikiwemo Tunguu – Makunduchi kilomita 53, Fumba – Kisauni kilomita 12, Mkoani - Chake Chake kilomita 43.5 pamoja na barabara ya Chake – Wete kilomita 22.1. Utekelezaji wa mradi huu hadi kufikia mwishoni mwa mwezi wa Machi, 2023 ni kama ifuatavyo:-

**i. Barabara ya Tunguu - Makunduchi, Fumba – Kisauni na Barabara ya Mkoani – Chake.**

42. **Mheshimiwa Spika,** Barabara hizi zitajengwa na Mkandarasi Kampuni ya PROPAV/MECCO JV ya nchini Hispania kwa mkopo kutoka "United Kingdom Export Finance – UKEF", kwa gharama ya Euro Milioni 230.7 ambapo tayari Wizara imeshasaini Mkataba wa Ujenzi wa barabara hizi tokea mwezi wa Septemba, 2022.

43. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa 2022/2023, Ujenzi wa barabara hizi ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 230,707,000,000. Kati ya fedha hizo TSH 28,947,000,000 ni kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na TSH 201,760,000,000 kutoka kwa Mfadhili. Hadi kufikia Machi, 2023 hakuna fedha iliyopatikana.

**ii. Barabara ya Wete - Chake km 22.1**

44. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea na ujenzi wa barabara ya Wete – Chake ambapo kazi za ujenzi wa barabara

hiyo inatekelezwa na Kampuni ya Mwananchi Engineering Company Limited (MECCO) kutoka Dar -es – Salaam chini ya usimamizi wa Mshauri Elekezi Dar al Handasah kwa ufadhili wa BADEA, SAUDI FUND na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Muda wa utekelezaji wa mradi huu ni miezi 30 na ulianza rasmi mwezi wa Februari 2022 na unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba 2024. Mradi huu unatarajiwa kutumia TSH Bilioni 23.6 kwa ajili ya ujenzi na USD 1,076,100 kwa ajili ya kazi za usimamizi wa mradi. Kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 jumla ya kilomita 10.5 zimefanyiwa usafi na kilomita 8.2 zimewekwa tabaka mbali mbali za kifusi. Aidha, Wizara kwa hatua za awali imekamilisha ulipaji wa fidia wa nyumba zitakazoathirika kutokana na ujenzi wa barabara hiyo kutoka Melitano hadi Limbani na kwa sasa kazi za ujenzi zinaendelea kama zilivyopangwa. Mradi huu umefikia asilimia 14 ya utekelezaji.

45. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa 2022/2023, ujenzi wa barabara hii ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 19,000,000,000. Kati ya fedha hizo TSH 9,000,000,000 ni kutoka Serikalini na TSH 10,000,000,000 ni kutoka BADEA na SAUDI FUND. Hadi kufikia Machi, 2023 jumla ya TSH 11,985,341,535 zimepatikana sawa na asilimia 63 ya makadirio ya bajeti. Kati ya fedha hizo, TSH 2,778,352,176.60 ni kutoka kwa Mfadhili (BADEA/SAUD FUND) na TSH 9,206,989,359 ni kutoka Serikalini kwa ajili ya malipo ya fidia na Mshauri Elekezi.

## MIRADI YA UIMARISHAJI WA USAFIRI WA ANGA

### d. Uwanja wa Ndege wa Pemba

46. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ina lengo la kuimarisha Uwanja wa Ndege wa Pemba kwa kuongeza urefu wa barabara ya

kutua na kurukia ndege (runway and taxi way), kujenga jengo jipya la abiria (Terminal Building) na miundombinu husika itakayowezesha uwanja huo kutua ndege aina ya Code C (Boeing 737-800) na zinazolingana. Aidha, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi imeshasaini Mkataba wa Ujenzi na Kampuni ya PROPAV/MECCO JV ya nchini Hispania.

47. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa 2022/2023, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 134,100,000,000 kati ya fedha hizo TSH 8,000,000,000 ni kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na TSH 126,100,000,000 ni kutoka kwa Mfadhili. Hadi kufikia Machi, 2023 hakuna fedha iliyopatikana.

**e. Uwanja wa Ndege wa Nungwi**

48. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi ina lengo la kuimarisha Uwanja wa Ndege wa Nungwi kwa kuutanua na kuuongezea miundombinu ili kuuwezesha kutua ndege aina ya Code C na kutumika wakati wote. Uwanja huu utasaidia kuimarisha huduma za safari kwa watalii pamoja na kuimarisha huduma za usafiri nchini. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ilipanga kufanya Upembuzi Yakinifu kwa ajili ya kuujenga upya uwanja huo utakaokidhi mahitaji ya sasa na baadae. Hata hivyo, kazi hii haikufanyika kutokana na kujitokeza Mwekezaji aliyeonesha nia ya kuwekeza katika Uwanja huo, kwa sasa Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege inaendelea na mazungumzo na Mwekezaji huyo na yapo katika hatua za awali.

49. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 6,600,000,000 kutoka Serikalini. Hadi kufikia Machi 2023, TSH 368,012,193 zimetumika sawa na asilimia 5.5 kwa ajili ya malipo ya Mshauri Elekezi wa Jengo la abiria Terminal III.

## MIRADI YA UIMARISHAJI WA USAFIRI WA BAHARINI

### f. Bandari Jumuishi ya Mangapwani

50. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imepanga kujenga Bandari Jumuishi Mangapwani inayojumuisha bandari ya Mafuta na Gesi, Bandari ya Mizigo (Makontena na Kichele) pamoja na Chelezo cha kufanyia matengenezo vyombo vya baharini. Wizara inaendelea kuweka miundombinu kwa ujenzi wa Barabara za ndani (Ring Road) katika eneo la mradi wa Bandari Jumuishi ya Mangapawani zenye urefu wa kilomita 12 kama zilivyoainishwa ndani ya Mpango Mkuu wa Bandari hiyo (Mangapwani Port Master Plan). Kazi za ujenzi wa barabara hizo zinatekelezwa na Kampuni ya ORKUN ambayo imepewa muda wa miezi kumi na nane (18) kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo.

51. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Bandari ya Mafuta na Gesi, jumla ya wawekezaji saba (7) wamejitokeza katika eneo la mafuta na gesi. Kati ya hao, watano (5) wamejitokeza kwa ajili ya kujenga Bohari za kuwekea mafuta na wawili (2) kwa ajili ya kujenga gati ya mafuta na Gesi. Kwa sasa Shirika la Bandari ikishirikiana na ZURA na ZPDC linaendelea kufanya mapitio ya nyaraka zilizowasilishwa na wawekezaji ili waweze kujiridhisha na hatimae kufanya maamuzi sahihi. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TSH 8,000,000,000 kutoka Serikalini. Hadi kufikia Machi 2023, TSH 481,183,926 zimetumika sawa na asilimia 6 kwa ajili ya malipo ya Mshauri Elekezi.

52. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia Programu ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji ilipangiwa kutumia jumla ya TSH 564,007,000,000 kwa kazi za Maendeleo. Kati ya fedha hizo, TSH 337,860,000,000 ni mkopo

kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TSH 226,147,000,000 ni mchango kutoka Serikalini. Hadi kufikia Machi, 2023, jumla ya TSH 72,971,447,148 zimetumika sawa na asilimia 13 ya makadirio. Kati ya fedha hizo, TSH 9,506,749,943 ni mkopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 4 ya makadirio, TSH 63,464,697,205 ni mchango wa Serikali sawa na asilimia 28 ya makadirio ya bajeti.

53. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ilipokea jumla ya TSH 6,728,397,766 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) ikiwa TSH 6,390,168,495 ni malipo ya mwisho kwa Mkandarasi Kampuni ya CCECC wa Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Bububu – Mahonda - Mkokotoni, Pale – Kiongele, Matemwe – Muyuni na Fuoni – Kombeni na TSH 338,229,271 ni malipo kwa Kampuni ya Rans ambayo inajenga soko la Mamalishe Kinyasini ikiwa ni sehemu utekelezaji mradi huo uliojumuisha ujenzi wa miradi ya huduma za kijamii ikiwemo ujenzi wa soko hilo. Fedha hizi zilitengwa katika bajeti ya mwaka wa fedha uliopita 2021/2022.

### C.3.2. PROGRAMU YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA)

54. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ina lengo la kuhakikisha kuwepo kwa miundombinu na huduma bora za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) Zanzibar. Matokeo yanayotarajiwa ni kuwepo kwa miundombinu na huduma bora za TEHAMA. Programu hii ina programu ndogo moja (1) ambayo ni Programu ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA.

### C.3.2.1. Programu Ndogo ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA.

**55. Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Idara ya Mawasiliano pamoja Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar (ZICTIA) na ina lengo la kuhakikisha kuwepo kwa miundombinu na huduma bora ya TEHAMA zilizo salama na endelevu. Kupitia programu hii ndogo Wizara imeweza kutekeleza yafuatayo:-

### 5. IDARA YA MAWASILIANO

**56. Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mawasiliano kupitia programu ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA ina jukumu la kuratibu huduma za mawasiliano ya simu, posta ikiwemo Anuani za makaazi na postikodi, mtandao (intaneti) pamoja na kusimamia maendeleo ya huduma za TEHAMA Zanzibar.

**57. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Idara ya Mawasiliano ilipanga kuratibu huduma za mawasiliano ya simu, intaneti pamoja na huduma za TEHAMA, kuratibu ujenzi wa minara 42 ya mawasiliano Unguja na Pemba, kutoa mafunzo na huduma za TEHAMA kwa wananchi Unguja na Pemba kupitia vituo vya TEHAMA jamii, kusimamia na kuratibu operesheni Anuani za Makaazi na posikodi pamoja na kujenga kituo cha TEHAMA jamii ili kuongeza huduma za TEHAMA kwa jamii.

**58. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Idara ya Mawasiliano imeratibu huduma za mawasiliano ya simu, intaneti pamoja na huduma za TEHAMA. Aidha, Idara kwa kushirikiana na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) imekamilisha mradi wa ujenzi wa Minara 42 ya Mawasiliano Unguja na Pemba ambapo jumla ya vijiji 80 na wananchi wapatao 300,000 wanaoishi katika maeneo hayo

wamenufaika na mradi huo. **Kiambatanisho nambari 8** kinahusika.

59. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana TCRA imefanya ukaguzi wa kubaini upatikanaji wa mawasiliano ya sauti na data Unguja na Pemba. Ukaguzi huo ulionesha kuwa katika kisiwa cha Unguja kati ya Shehia 259, Shehia 255, sawa na asilimia 98.5 zimefikiwa na huduma ya mawasiliano ya sauti na data na Shehia 4 sawa na asilimia 1.5 zina changamoto ya upatikanaji wa huduma za mawasiliano. Shehia hizo ni Moga, Miwani, Ng'ambwa na Pete. Kwa upande wa Pemba matokeo ya ukaguzi yanaonesha kuwa, kati ya Shehia 129, Shehia 117 sawa na asilimia 90.7 zimefikiwa na huduma ya mawasiliano ya sauti na data. Shehia 12 sawa na asilimia 9.3 zina changamoto ya mawasiliano, shehia hizo ni Kinyasini, Piki, Mlindo, Kifundi, Tondooni, Uwandani, Michungwani, Kiwani, Mgogoni, Maziwani, Shumba Viamboni na Wingwi Njuguni.

60. **Mheshimiwa Spika,** Aidha, Wizara ilifanya ukaguzi wa kubaini upatikanaji wa huduma za Mawasiliano katika Visiwa vidogo vidogo Unguja na Pemba. Kwa upande wa Pemba ilibainika visiwa 8 kati ya Visiwa 26 vina changamoto ya huduma za mawasiliano, visiwa hivyo ni:- Kashani, Vikunguni, Vijiwe vitatu, Mapanya, Uvinje, Kokota, Matumbi na Funzi. Kwa upande wa Unguja ilibainika visiwa 2 kati ya visiwa 18 vina changamoto ya huduma za mawasiliano, visiwa hivyo ni Mwana wa Mwana na Niamembe.

61. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mawasiliano imefanikiwa kutoa mafunzo na huduma za TEHAMA kwa wananchi wapatao 2,056 kupitia vituo vya TEHAMA jamii vilivyopo katika kila Wilaya Unguja na Pemba. Aidha, Wizara imekamilisha mradi wa kujenga kituo chengine cha TEHAMA katika Wilaya ya

Magharibi B Skuli ya Bwefum na tayari kituo hicho kinaendelea kutoa huduma za TEHAMA kwa wananchi katika eneo hilo.

62. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kusimamia na kuratibu operesheni Anuani za Makaazi ambapo katika kuhakikisha mfumo wa Anuani za Makaazi unaimarika, Wizara inaendelea na zoezi la kufanya uhakiki ili kurekebisha changamoto zilizojitokeza wakati operesheni. Kulingana na uhakiki unaoendelea kufanyika Zanzibar takwimu zinaonesha kwamba hadi Machi 2023 jumla anuani 528,417 zimesajiliwa katika Mfumo wa NaPA ambapo anuani 78,309 zimeongezeka kutoka 450,108 sawa na ongezeko la asilimia 17.40.

63. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Idara ya Mawasiliano kupitia programu ndogo ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA ilipangiwa kutumia jumla ya TSH 1,091,540,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, TSH 350,640,000 ni mshahara na TSH 740,900,000 ni kwa ajili matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2023, jumla ya TSH 411,556,857 zimetumika sawa na asilimia 37 ya makadirio ya bajeti. Kati ya fedha hizo, TSH 225,531,157 ni mshahara na TSH 186,025,700 ni matumizi mengineyo.

## 6. WAKALA WA MIUNDOMBINU YA TEHAMA ZANZIBAR (ZICTIA)

64. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA (ZICTIA) kupitia programu ndogo ya miundombinu na huduma za TEHAMA imepewa jukumu la kusimamia na kuendesha Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano wa Zanzibar, kusimamia kituo kikuu cha kuhifadhia taarifa (Data Center) cha Serikali pamoja na Minara ya mawasiliano ya simu.

65. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA ilipanga kuviunganisha

na Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano vituo 60 vya taasisi mbalimbali za Serikali Unguja na Pemba na hadi kufikia mwezi wa Machi, 2023 ZICTIA imefanikiwa kuviunganisha na Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano vituo 53 vya Taasisi za Serikali sawa na asilimia 88 kwa makadirio ya mwaka Unguja na Pemba. **Kiambatanisho nambari 9A** kinahusika.

66. **Mheshimiwa Spika,** ZICTIA imefanya matengenezo ya Mkonga katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba yakiwemo eneo la Tunguu, Marumbi, Unguja Ukuu, Shirika la Magazeti- Maisara, Chukwani, Fumba, Amani na Mombasa SOS, KwaAlamsha, Masingini, Dole, Kizimkazi, Mbweni, Makunduchi, Mtoni na Binguni kwa Unguja. Kwa upande wa Pemba matengenezo yamefanyika katika eneo la Ikulu – Pagali. Matengenezo hayo yamesababishwa na hujuma za Makusudi za baadhi ya Wananchi, kuliwa na wadudu (Panya) pamoja na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Sambamba na hilo, ZICTIA inaendelea kuimarisha huduma katika vituo vya mkonga (POP) kwa kufanya maboresho (Services), Vipoza hewa (AC) na Majenereta ya vituo vyote Kumi na Mbili (12) Unguja na Pemba. Pia, ZICTIA imefanikiwa kusaini Mikataba Minne (4) na Wawekezaji wenye nia ya kuekeza katika Sekta ya Mawasiliano hususan katika miundombinu ya TEHAMA, ikiwemo kuweka njia ya Mkonga wa Kimataifa wa Baharini (International Gateway) na kuanzisha Mji wa TEHAMA Zanzibar (Cyber City).

67. **Mheshimiwa Spika,** ZICTIA ilipanga kuendelea kuhifadhi mifumo kutoka Taasisi mbalimbali katika kituo cha kuhifadhia taarifa (Data Centre). Hadi kufikia Machi 2023, ZICTIA imefanikiwa kupokea na kuihifadhi katika Kituo hicho mifumo mipya 12 kutoka katika Taasisi mbali mbali. **Kiambatanisho nambari 9 B** kinahusika.

68. **Mheshimiwa Spika,** ZICTIA ilipanga kuendelea na mradi wa uimarishaji kituo cha kutunzia taarifa. Hadi kufikia Machi 2023 ZICTIA imefanikiwa kukamilisha mradi wa uimarishaji kituo hicho na kuwa kituo cha kwanza nchini Tanzania chenye hadhi ya "Software Define" na kupelekea kuimarika kwa huduma zinazopatikana kutoka katika kituo hicho ikiwemo usalama wa taarifa zinazohifadhiwa pamoja na kuwahakikishia wateja (Taasisi) juu ya upatikanaji wa huduma bora za "Data Center". Aidha, kazi ya Upembuzi Yakinifu na tathmini ya mazingira kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa kituo mbadala cha kuhifadhia taarifa zinaendelea. Mradi huu unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT).

69. **Mheshimiwa Spika,** Pia, Wakala ilipanga kutoa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa wafanyakazi kumi na tano15. Hadi kufikia Machi, 2023 jumla ya wafanyakazi kumi na moja (11) walipatiwa mafunzo hayo katika vyuo mbali mbali nchini kwa lengo la kuwaongezea ufanisi katika maeneo yao ya kazi sawa na asilimia 73 ya wafanyakazi waliopangwa kupatiwa mafunzo hayo kwa mwaka. Mafunzo hayo yanajumuisha ufuatiliaji na tathmini, utawala na uendeshaji, matengenezo ya zana na vifaa vya mawasiliano. Pia, ZICTIA imewapatia wafanyakazi wanne (4) mafunzo ya upigaji dawa ya kuondoa wadudu (Fumigation) katika kituo cha kuhifadhia taarifa (Data Center) pamoja maeneo ya vituo vyote vya Mkonga Unguja na Pemba.

70. **Mheshimiwa Spika,** ZICTIA pia ilitoa uelewa kwa jamii kuhusiana na huduma zinazotolewa na ZICTIA pamoja na umuhimu wa matumizi na uhifadhi wa miundombinu ya TEHAMA. Mafunzo hayo yametolewa kupitia vyombo vya habari pamoja na Tamasha la Tisa (9) la Biashara lililofanyika katika viwanja vya Maisara.

71. **Mheshimiwa Spika,** ZICTIA imeanza rasmi kazi ukusanyaji wa mapato yanayotokana na huduma za Mtandao (Internet Fees) zinazotolewa kwa Taasisi za Serikali, Mashirika, Mamlaka na Taasisi nyengine zinazojitegemea.

72. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, ZICTIA ilikadiria kukusanya jumla ya TSH 2,196,712,495 kupitia vyanzo vyake vya mapato. Hadi kufikia Machi, 2023 jumla ya TSH 1,141,717,006 zimekusanywa sawa na 51.97 za makadirio. Aidha, ZICTIA imekusanya jumla ya TSH 2,017,567,139 zinazotokana na malipo ya huduma ya uendeshaji na matengenezo (Operation and Maitainance). Kati ya hizo, TSH 1,072,469,260 zimetumika sawa na asilimia 53 ya makusanyo.

73. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa Fedha 2022/2023, Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA kupitia programu ndogo ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA ilipangiwa kutumia jumla ya TSH 2,395,084,261 kwa kazi za kawaida, ikiwa TSH 571,384,261 ni ruzuku ya mshahara na TSH 1,823,700,000 ni ruzuku kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia machi 2023, jumla ya TSH 2,378,528,894 zimetumika sawa na asilimia 99.3 ya makadirio. Kati ya fedha hizo, TSH 558,118,185 ni mshahara na TSH. 1,820,410,709 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ikiwemo malipo ya Mkandarasi wa uimarishaji wa Kituo cha kuhifadhia taarifa (Data Center).

### C.3.3. PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI

74. **Mheshimiwa Spika,** progamu hii ina lengo la kuhakikisha kuwa Wizara inaratibu na kutayarisha Sera na Mipango bora katika Sekta ya Mawasiliano na Usafirishaji pamoja na usimamizi mzuri wa rasilimali watu. Programu hii ina programu ndogo tatu (3) ambazo ni:- Usimamizi wa Utawala

na Uendeshaji, Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara pamoja na Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba.

#### C.3.3.1. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji

75. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi ambayo imepewa jukumu la kusimamia na kutathmini shughuli za uendeshaji wa Wizara na kushughulikia maslahi pamoja na nidhamu kwa wafanyakazi. Aidha, Idara inaandaa na kusimamia Mpango wa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa wafanyakazi wa Wizara pamoja na utunzaji wa kumbukumbu na mali za Wizara. Pia, Idara inajukumu la kuimarisha mazingira mazuri ya utendaji kazi kwa kuhakikisha vitendea kazi vinapatikana kwa wakati. Vilevile, Idara inatoa huduma za ununuzi na usimamizi wa mapato na matumizi ya Wizara.

76. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Idara ya Uendeshaji na Utumishi kupitia programu ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji ilipanga kuwajengea uwezo wafanyakazi 52 wa Wizara kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ili waweze kutoa huduma bora na kwa ufanisi. Aidha, Idara Idara ilipanga kuimarisha huduma za kiutawala na utumishi ikiwemo kuweka mazingira mazuri ya kazi, kusimamia maslahi ya watumishi pamoja na kuongeza vitendea kazi kwa lengo la kuleta ufanisi.

Kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imefanikiwa kuwapatia mafunzo mbalimbali wafanyakazi 51 Unguja na Pemba sawa na asilimia 98 ya wafanyakazi waliopangwa kupatiwa mafunzo hayo. Kati ya hao, wafanyakazi 9 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi tofauti katika Vyuo vya ndani na Nje ya nchi na wafanyakazi 42 wamepatiwa mafunzo ya muda

mfupi katika kozi tofauti. **Kiambatanisho nambaRI 10A na 10B** kinahusika.

Aidha, Idara imefanikiwa kutoa mafunzo ya ndani yanayohusu Haki na Wajibu kwa Watumishi 81 wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kutoka katika Idara tatu ikiwemo Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti pamoja na Idara ya Mawasiliano.

Katika kuhakikisha mazingira mazuri ya kufanyia kazi kwa watendaji yanaimarishwa, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imezifanyia matengenezo Ofisi, kuimarisha vitendea kazi kwa kununua vifaa vya Ofisi pamoja na kuwapatia wafanyakazi stahiki zao ikiwemo malipo ya mishahara, malipo ya likizo, malipo baada ya saa za kazi pamoja na kuwapanga wafanyakazi katika madaraja yao. Aidha, Idara imefanya mapitio ya Mpango wa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa lengo la kuwa na utaratibu bora wa kuwejengea uwezo wafanyakazi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

77. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Idara ya Uendeshaji na Utumishi kupitia programu ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji ilipangiwa kutumia jumla ya TSH 2,896,608,117 kwa kazi za kawaida, ikiwa TSH 1,300,896,117 ni mshahara na TSH 1,595,712,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2022, jumla ya TSH 1,609,323,088 zimetumika sawa na asilimia 55.5 ya makadirio ya Bajeti. Kati ya fedha hizo, TSH 1,184,427,262 ni Mishahara na TSH 424,895,826 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

### C.3.3.2. Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara

78. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ambayo imepewa jukumu la

kupanga, kuratibu, kusimamia na kutathmini utekelezaji wa Sera na Mipango ya sekta za Usafiri na Mawasiliano. Aidha, Idara inaratibu kazi zote za maendeleo ya Wizara ikiwemo kubuni, kutayarisha na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Pia, Idara inajukumu la kubuni na kufanya tafiti za kisekta ikiwemo ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu.

79. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara ilipanga kuendelea kuratibu na kufanya Tafiti za Wizara, kuzifanyia mapitio Sera ya Usafiri ya mwaka 2008 na Sera ya TEHAMA ya mwaka 2013 ili ziendane na mahitaji ya sasa. Vilevile, Idara ilipanga kuratibu na kusimamia miradi ya maendeleo, kukusanya takwimu mbalimbali katika sekta zinazosimamiwa na Wizara, kuratibu Taasisi na Mashirika yanayojitegemea yaliyo chini ya Wizara, kuratibu na kufanya vikao vya ushirikiano baina ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi (SMZ), Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (SMT) pamoja na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (SMT), kutoa mafunzo kwa watendaji wake yanayohusiana na utayarishaji wa bajeti katika mfumo wa programu (PBB), ufuatiliaji na tathmini, namna ya kufanya tafiti pamoja na usimamizi wa miradi kwa lengo la kuwajengea uwezo katika kutekeleza majukumu yao.

Kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imefanikiwa kuendelea kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kukusanya takwimu zinazohusu Wizara, kutayarisha ripoti mbalimbali za utekelezaji wa kazi za Wizara pamoja na kuanza kuifanyia mapitio Sera ya Taifa ya Usafiri ya mwaka 2008 na sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2013 ambayo kazi hiyo inaendelea na ipo katika hatua za kupata maoni ya wadau. Pia, Idara imeandaa Rasimu ya Muongozo wa ukusanyaji

wa takwimu za Wizara (Statistical Guidelines) kwa lengo la kuongeza ufanisi na kurahisisha ukusanyaji na utoaji wa ripoti za takwimu.

80. **Mheshimiwa Spika,** Idara pia inaendelea kuratibu Taasisi na Mashirika mbalimbali yanayojitegemea yaliyo chini ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi pamoja na kuratibu na kuandaa vikao vitatu vya ushirikiano baina ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi – SMT, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari - SMT, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi - SMZ pamoja na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi - SMZ vinavyohusu Sekta ya uchukuzi, Mawasiliano na Ujenzi. Vikao hivi vimesaidia sana katika kubadilishana uzoefu wa kazi pamoja na kutatua changamoto mbalimbali ambazo zilikuwa zinaikabili sekta hizo.

Aidha, Idara imeweza kuwapatia mafunzo ya muda mfupi watendaji wake na wa Taasisi mbalimbali kuhusiana na utekelezaji wa miradi kwa njia ya ubia baina ya Serikali na Sekta binafsi (PPP) na taratibu za ujenzi, manunuzi na fedha (EPC+F).

81. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanya mapitio ya Sheria mbalimbali za sekta ya Usafiri na Mawasiliano ikiwemo Sheria ya Uwanzishwaji wa Shirika la Mawasiliano Zanzibar 2023 na Marekebisho Sheria Namba 5 ya Usafiri wa Baharini ya Mwaka 2006 (Maritime Transport Act no.5 of 2006).

82. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara ilipangiwa kutumia jumla ya TSH 1,030,728,000 kwa kazi za kawaida, ikiwa TSH 330,040,000 ni mshahara na TSH 700,688,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2022, jumla ya TSH 401,623,670 zimetumika sawa na asilimia 38.9

ya makadirio ya bajeti. Kati ya fedha hizo, TSH 240,908,691 ni mishahara na TSH 160,714,979 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

### C.3.3.3.Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba

83. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Ofisi Kuu – Pemba ambayo imepewa jukumu la kuratibu na kusimamia kazi zote za Wizara kwa upande wa Pemba. Kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Ofisi Kuu Pemba imeratibu na kusimamia maslahi ya wafanyakazi ikiwemo malipo ya likizo, malipo baada ya saa za kazi pamoja na kulipia huduma nyengine mbali mbali. Pia, Ofisi imeweka mazingira bora ya kazi kwa kununua vifaa vya kuendeshea Ofisi pamoja na kufanya matengenezo madogo madogo ya Ofisi. Aidha, Ofisi Kuu imeweza kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi 2 na muda mfupi wafanyakazi 7 katika fani mbalimbali. Kwa ujumla Ofisi Kuu Pemba imeratibu kwa ufanisi kazi zote zinazofanywa na Wizara kwa upande wa Pemba.

84. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi Kuu Pemba kupitia programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba ilipangiwa kutumia jumla ya TSH 1,040,954,000 kwa kazi za kawaida, ikiwa TSH 437,334,000 ni mshahara na TSH 603,620,000 ni kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2023, jumla ya TSH 513,291,660 zimetumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 49.3 ya makadirio ya bajeti. Kati ya fedha hizo, TSH 363,849,660 ni mshahara na TSH 149,442,000 ni matumizi mengineyo.

## D. UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA KWA KIPINDI CHA JULAI, 2022 HADI MACHI, 2023 PAMOJA NA MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

85. **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa bajeti kwa Taasisi zinazojitegemea kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 na malengo yanayotarajiwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ni kama ifuatavyo:-

### D.1. SHIRIKA LA BANDARI ZANZIBAR

86. **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Bandari lina jukumu la kutoa huduma za uingizaji na utoaji meli katika Bandari za Unguja na Pemba, ufungaji na ufunguaji wa meli kwenye gati, uangalizi wa alama za kuongozea usafiri wa meli (minara na maboya), uteremshaji na upakiaji wa bidhaa kwenye meli pamoja na vyombo vyengine vya usafiri wa baharini. Kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Shirika la bandari limefanikiwa kutekeleza yafuatayo.

87. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa kazi za kawaida, Shirika lilipanga kuhudumia vyombo, mzigo, abiria na makontena katika bandari zake Unguja na Pemba. Kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Shirika limehudumia vyombo mbali mbali vya mizigo na abiria katika Bandari zake. Jumla ya meli za Kigeni 92 (GRT 1,104,035) zimehudumiwa sawa na asilimia 93 ya meli 98 (GRT 1,334,571) zilizopangwa kuhudumiwa katika kipindi hicho. Kwa upande wa meli za ndani, jumla ya meli 3,470 zilihudumiwa sawa na asilimia 74 ya meli 4,700 zilizopangwa kuhudumiwa katika kipindi hicho.

Pia, Shirika limehudumia majahazi na maboti ya vyuma 7,519 sawa na asilimia 63 ya majahazi na maboti ya vyuma 12,000

yaliopangwa kuhudumiwa. Kwa upande wa huduma za mizigo, Shirika limehudumia jumla ya tani 575,616 za mzigo wa meli ikiwa ni sawa na asilimia 59 ya tani 970,000 za mzigo zilizopangwa kuhudumiwa. Vile vile, Shirika limehudumia Tani 354,854 za mizigo ya majahazi sawa na asilimia 99 ya tani 355,000 zilizopangwa kuhudumiwa katika kipindi hicho.

88. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Makontena, Shirika limehudumia Makontena 38,519 (Teus 53,035) sawa na asilimia 60 ya makadirio ya makontena 64,198 (Teus 88,391) yaliyopangwa kuhudumiwa katika kipindi hicho. Aidha, Shirika lilipanga kuhudumia tani 145,000 za mafuta ya kuwasha (Petrolium product) na hadi kufikia machi, 2023 jumla ya tani 110,558 zimehudumiwa sawa na asilimia 76 ya makadirio kwa kipindi hicho.

89. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa miradi, Shirika la Bandari kwa kipindi Julai, 2022 hadi Machi, 2023 limetekeleza miradi ifuatayo:-

**a. Uimarishaji wa Bandari ya Malindi**

90. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu una lengo la kuimarisha bandari ya Malindi ili kupunguza msongamano wa makontena katika bandari hiyo. Kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, kazi zilizofanyika ni kama ifuatavyo:-

i. Kukamilisha kazi ya uchimbaji wa mchanga katika Gati nambari 3 kwa lengo la kuongeza kina cha maji hadi kufikia mita sita (6) kwenda chini (low tide) kwa ajili ya kupata eneo jengine la kuegeshea meli ambapo kwa sasa meli ndogo zenye urefu wa mita 100 zinafunga katika eneo. Jumla ya TSH. 622,625,191 zimetumika kwa ajili yakukamilisha kazi hiyo.

ii. Kukamilisha ujenzi wa bandari kavu (ICD) katika eneo la Bwawani lenye ukubwa wa mita za mraba 4,000 ambalo linauwezo wa kuhifadhi makontena 320. Hivyo, kwa sasa kazi ya utoaji mizigo (distuffing) katika makontena zimehamishiwa katika eneo hilo. Jumla ya TSH 1,207,109,000 zimetumika kwa ajili ya ujenzi huo.

iii. Kukamilisha ukarabati wa eneo la Maruhubi lenye ukubwa wa mita za mraba 10,000 ambalo lina uwezo wa kuhifadhi makontena matupu zaidi ya 1,200. Eneo hilo limeanza kutumika kwa ajili ya kazi hiyo na jumla ya TSH.169,046,124 zimetumika kwa kazi hiyo.

**b. Uimarishaji wa Bandari ya Mkokotoni.**

**91. Mheshimiwa Spika,** Shirika limepanga kuimarisha Bandari ya Mkokotoni kwa kujenga Gati, barabara za ndani, ghala la kuhifadhia mizigo, jengo la kupumzikia abiria, njia ya waenda kwa miguu pamoja na njia ya kuingia na kutoka meli (Approaching Channel). Mradi huu ulipangwa kutekelezwa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza ulihusisha ujenzi wa Gati ya Mkokotoni ambapo kazi hiyo imekamilika. Awamu ya pili ilihusisha ujenzi wa njia ya abiria wanaoenda kwa miguu pamoja na jengo la kupumzikia abiria lenye uwezo wa kuhifadhi abiria 250 ambapo kazi hizo zimefikia asilimia 90 ya utekelezaji. Kazi za ujenzi huo zinatekelezwa na Kampuni ya Edge na hadi kufikia machi, 2023 jumla ya TSH. 774,360,814 zimetumika.

**c. Ujenzi wa Bandari ya Shumba Mjini**

**92. Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unajumuisha ujenzi wa Gati, ghala la kuhifadhia mizigo, jengo la kupumzikia abiria la ghorofa 2 pamoja na njia ya kuingia na kutoka meli (Approaching Channel) kwa gharama ya TSH 5,772,506,880. Kwa mwaka wa fedha, 2022/2023, Shirika limepanga kuanza

ujenzi wa Gati yenye urefu wa mita 45 na upana wa mita 20 na itakuwa na uwezo wa kuhudumia meli zenye uzito GRT (Gross Rated Tonnage) 2000. Kazi za ujenzi zinafanywa na Kampuni ya Comfix & Engineering Smart Solution. Aidha kazi za ujenzi zimeanza kwa kwa kusafisha eneo na kujenga uzio (Mobilization and Site establishment) pamoja na kufanya thathmini katika eneo hilo. Kwa ujumla mradi huu umefikia asilimia 30 na jumla ya TSH 1,731,752,064 zimetumika.

**d. Uimarishaji wa Bandari ya Mkoani**

**93. Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unatekelezwa na Mkandarasi China Railway Bridge Engineering Company LTD unaojumuisha matengenezo ya njia ya kupitia vyombo vya kutendea kazi bandarini, kujenga njia ya waendao kwa miguu, kuliimarisha eneo la kuwekea makontena, ujenzi wa uzio na ujenzi wa ukuta wa kuzuia mmong'onyoko. Kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi 2023, kazi za ujenzi katika eneo la kuhifadhia makontena (Container Yard) lenye mita za mraba 4,200 na uzio wenye urefu wa mita 290 pamoja na mfumo wa usalama wa umeme zimekamilika.

Pia, Shirika limekamilisha matengenezo ya njia itakayopitishia vitendea kazi kama vile Reach Stacker, Crane na Terminal Tractor kwa kuitanua pamoja na kujenga upya njia ya wapita kwa miguu yenye upana wa mita mbili na nusu (2.5) na urefu wa mita 300 kwa lengo la kuongeza usalama wa abiria pamoja na kuwakinga kutokana na jua na mvua. Aidha, Shirika limekamilisha ujenzi wa ukuta wa kuzuia mmng'onyoko wa udongo (Retaining Wall) pamoja na kuboresha Gati (Jetty) kwa kuziba nyufa na kurekebisha zege iliyoharibika. Kwa ujumla mradi huu umetumia TSH 3,148,954,026.19 na umefikia asilimia 90 ya utekelezaji.

### e. Ujenzi wa Bandari ya Wete

94. **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Bandari imepanga kuijenga upya bandari ya Wete ili iweze kuhudumia meli za Makontena na mizigo. Shirika limeanza kufanya kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu kupitia Mshauri elekezi Inros Lackener kutoka Ujerumani ambapo taarifa ya awali ameshaiwasilisha na kazi hiyo imefikia asilimia 48.

### f. Kuimarisha Vifaa vya Kufanyia Kazi Bandarini

95. **Mheshimiwa Spika,** Shirika linaendelea kuimarisha vifaa vya kufanyia kazi bandarini ili kuleta ufanisi wa kuhudumia mizigo na vyombo katika bandari za Unguja na Pemba. Hadi kufikia Machi, 2023 Shirika limenunuwa vifaa mbalimbali vya kufanyia kazi bandarini na tayari vimeshapokelewa na kuanza kutumika. Vifaa hivyo ni; Mobile crane yenye tani 60, Reach Stacker 3, Mobile Habor Crane ya tani 124, Terminal tractor, Winch Truck, mizani 4, scanner 1, generator 1, spreader 4 (20ft mbili na 40ft mbili), Reach stacker pamoja na Empty Reach Stacker. Jumla ya TSH 4,475,515,162 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa hivyo.

### g. Uimarishaji wa Mifumo ya TEHAMA Katika Shirika la Bandari.

96. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu una lengo la kuweka mfumo wa E - Port katika maeneo makuu matatu ambayo ni:- huduma za vyombo vya baharini, huduma za mizigo pamoja na huduma za utawala na uendeshaji wa Taasisi. Kwa sasa Shirika linaendelea kuweka Mfumo wa Tehama (E - Port) ambao una module kuu 5 zikiwemo (ERP- Enterprises Resources Planing) ambayo italeta ufanisi katika kusimamia shughuli zote za kiutawala na uendeshaji wa Shirika, Module ya 2 itahusisha usimamizi na uongozaji wa vyombo vya baharini (Vessel tracking system), Module ya 3 itahusisha usimamizi wa huduma za mizigo

(Terminal Operating System), moduli ya 4 itasaidia kuboresha ufanisi katika usimamizi wa matumizi ya mafuta katika Shirika (Fleet and Fuel Management System) na moduli ya 5 inaunganisha moduli zote na kutoa muhtasari wa ripoti juu ya shughuli zote za kiutendaji. Mifumo hii itakuwa inafanya kazi katika bandari zote 5 (Malindi, Mkokotoni, Mkoani, Wete na Wesha) pamoja na zile 3 zinazotarajiwa kujengwa ikiwemo ya Mangapwani, Shumba Mjini na Kizimkazi. Kazi ya uwekaji wa mifumo hiyo inafanywa na Kampuni ya Fortris ikishirikiana na Warsila Company. Jumla ya TSH 4,599,048,050 zimetumika kwa ajili ya kununua vifaa pamoja na malipo ya asilimia 30 kwa kampuni hizo. Mradi huu umefikia asilimia 60 ya utekelezaji.

**Mapato na Matumizi**

**97. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Shirika la Bandari lilikadiria kukusanya jumla ya TSH 53,770,651,303 kupitia katika vyanzo vyake mbalimbali na kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Shirika lilikadiria kukusanya jumla ya TSH 41,220,325,592. Hadi kufikia Machi, 2023, jumla ya TSH 31,269,911,749.87 zimekusanywa sawa na asilimia 76 kwa makadirio ya miezi tisa na asilimia 76 ya makadirio kwa mwaka.

Kwa upande wa matumizi, Shirika la Bandari kwa mwaka wa fedha 2022/2023 lilipanga kutumia jumla ya TSH 58,924,448,630 kwa kazi za kawaida na maendeleo. Kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Shirika lilipanga kutumia jumla ya TSH 38,357,543,572. Hadi kufikia Machi, 2023, jumla ya TSH 28,870,387,325 zimetumika sawa na asilimia 75 ya makadirio kwa kipindi cha miezi tisa na asilimia 49 kwa makadirio ya bajeti kwa mwaka. Kati ya fedha hizo, TSH. 5,413,508,641 ni mshahara, TSH. 13,686,391,564 ni matumizi mengineyo na TSH. 9,770,487,120 ni kwa ajili ya kazi za Maendeleo.

## MALENGO YA SHIRIKA LA BANDARI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

98. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024 Shirika la Bandari limepanga kuhudumia jumla ya meli 140 za kigeni zenye uzito (GRT) wa tani 2,066,558, Meli za ndani zipatazo 4,800 na Majahazi 12,300. Aidha, kwa upande wa huduma za mizigo, Shirika linatarajia kuhudumia tani 1,429,478 za mzigo mchanganyiko kwa meli za ndani na nje, makontena 68,820 (TEUs 90,565), tani 140,000 za mafuta ya kuwasha (Petroleum Fuel) pamoja na tani 375,000 za mzigo wa majahazi.

99. **Mheshimiwa Spika,** Pia, Shirika limepanga kuendelea kukamilisha miradi inayoendelea ambayo ilianza utekelezaji wake katika kipindi cha mwaka wa fedha uliopita, ikiwemo kukamilisha mradi wa uimarishaji wa Bandari ya Mkokotoni kwa kutengeneza njia ya kuingia na kutoka meli (Approaching Channel) pamoja na kubadilisha muelekeo wa maji, Ujenzi wa Bandari ya Shumba Mjini ikiwemo kuongeza kina cha maji pamoja na kutengeneza njia ya kuingia na kutoka meli (Approaching Channel), kujenga bandari kavu ya muda pamoja na kuendelea kuimarisha Bandari ya Mkoani kwa kujenga jengo la ofisi, jengo la abiria pamoja na sehemu ya kuhifadhia mafuta.

Aidha, kwa upande wa Bandari ya Kizimkazi, Shirika limepanga kufanya Upembuzi Yakinifu kwa lengo la kuanza maandalizi ya ujenzi wa bandari hiyo. Pia, Shirika la Bandari limepanga kufanya ukarabati wa minara ikiwemo mnara wa makunduchi, mwanamwana, ukarabati wa becon maruhubi juu na chini, ukarabati wa becon bet-el-ras juu ili kuimarisha huduma za bandari.

Vilevile, Shirika limepanga kununua vifaa mbalimbali ili kuimarisha huduma za bandari, vifaa hivyo ni:- terminal trekta, fork lift ya tani 16, ununuzi wa gari, mashine ya upekuzi wa mizigo, maboya 7 ya kuongozea meli, vifaa vya TEHAMA pamoja na vifaa vya kudhibiti umwagikaji wa mafuta Baharini (Oil Spill Equipment).

Aidha, Shirika limepanga kuwajengea uwezo wafanyakazi mbalimbali kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ili waweze kufanyakazi zao kwa ufanisi.

**Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2023/2024**

**100. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Shirika la Bandari Zanzibar limekadiria kukusanya jumla ya TSH 53,889,470,192 na kutumia jumla ya TSH 93,663,578,661. Kati ya fedha hizo, TSH 20,560,611,052 kwa kazi za kawaida, TSH 7,819,268,464 mshahara na TSH 63,871,559,475 kwa kazi za maendeleo. Aidha, Shirika linategemea kuchukuwa mkopo wa TSH 50,000,000,000 ili kufanikisha utekelezaji wa miradi iliyopangwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

## D.2. SHIRIKA LA MELI ZANZIBAR

**101. Mheshimiwa Spika,** Shirika la Meli Zanzibar linamilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa asilimia Mia Moja. Shirika hili lilianzishwa rasmi chini ya Sheria nambari 3 ya mwaka 2013 (The Zanzibar Shipping Corporation Act, 2013) na limepewa jukumu la kuzisimamia na kuziendesha meli zote za Serikali pamoja na kutoa huduma za Uwakala kwa meli za kigeni zinazoingia katika Bahari ya Zanzibar.

**102. Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2023, Shirika la Meli Zanzibar limefanikiwa kufunga mkataba na

Kampuni ya Kookje Engineering ya Korea tarehe 16 Machi 2023 kwa ajili ya matengenezo ya meli ya MV Mapinduzi II kwa gharama ya dola za Kimarekani 3,875,797. Matengenezo hayo yameshaanza na yanatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi wa Septemba, 2023. Matengenezo ya meli hii yanahusisha mashine kuu mbili, vinu vya umeme, mfumo wa umeme, viyoyozi na maji taka. Aidha, Meli itapelekewa chelezoni Mombasa kwa ajili ya kuangalia hali ya chini baada ya kumalizika matengenezo hayo. Aidha, meli ya MT Ukombozi II inaendelea kufanya kazi zake za kusafirisha nishati ya mafuta ambapo kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 imefanya safari 28 na kusafirisha tani za mafuta 84,248.

**103. Mheshimiwa Spika,** Shirika pia linaendelea na kazi ya kutoa huduma za uwakala wa Meli. Hadi kufikia Machi, 2023, jumla ya meli 258 za kigeni zimehudumiwa kati ya Meli 291 zilizopangwa kuhudumiwa sawa na asilimia 89 ya makadirio. Meli hizo ni pamoja na meli za makontena, gesi, kichele na kitalii. **Kiambatanisho nambari 11** kinahusika.

**Mapato na Matumizi**

**104. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Shirika la Meli Zanzibar lilikadiria kukusanya jumla ya TSH 11,652,474,000, na kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Shirika lilikadiria kukusanya jumla ya TSH 9,075,289,200 kupitia vyanzo vyake mapato. Hadi kufikia Machi 2023 jumla ya TSH 8,374,772,946 zimekusanywa sawa na asilimia 92.6 ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 72 ya makadirio ya mwaka.

Kwa upande wa matumizi, Shirika lilipanga kutumia jumla ya TSH10,897,811,283 kwa kazi za kawaida na maendeleo. Ikiwa TSH 7,366,617,453 ni matumizi mengineyo, TSH

2,023,553,830 ni mshahara na TSH 1,507,640,000 ni kwa kazi za Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2023, jumla ya TSH 7,388,763,222 zimetumika sawa na asilimia 84 ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 68 ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo TSH 7,218,408,961 ni matumizi mengineyo, TSH 1,618,843,064 ni mishahara na TSH 587,066,689 ni ni kwa ajili ya kazi za maendeleo.

**105. Mheshimiwa Spika,** Shirika limekusanya TSH 1,127,265,095 ikiwa ni mapato yatokanayo na uuzaji wa meli ya MT Ukombozi na MV Maendeleo pamoja na makusanyo ya mapato ya TSH 7,760,000 yatokanayo na mauzo ya vifaa chakavu.

**MALENGO YA SHIRIKA LA MELI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024**

**106. Mheshimiwa Spika,** Shirika la Meli kwa mwaka wa fedha 2023/2024 limepanga kuendelea kuitengeneza meli ya MV Mapinduzi II, kusafirisha abiria 38,400 na mizigo tani 12,000 baina ya Unguja na Pemba. Aidha, Shirika limepanga kuanza ujenzi wa boti mbili za mwendo kasi zitakazokuwa na uwezo wa kusafirisha abiria 650 kila moja. Boti hizi zitafanya kazi ya usafirishaji abiria baina ya Unguja, Pemba, Tanga na Dar es salaam. Kwa upande wa Uwakala, Shirika limepanga kuhudumia jumla ya meli za kigeni 301 zikiwemo za makontena, mizigo mchanganyiko, meli za gesi na meli za watalii.

Pia Shirika limepanga kuwajengea uwezo wafanyakazi wake baada ya kukamilika kwa tathmini ya mahitaji ya mafunzo ya Shirika, kuandaa Mpango Mkakati wa Shirika pamoja na kuyafanyia matengenezo majengo ya Afisi Makao makuu, Pemba na Dar es Salaam.

**Makadirio ya Bajeti ya Mwaka wa fedha 2023/2024**

107. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Shirika limepanga kukusanya jumla ya TSH 12,539,656,218 kupitia vyanzo vyake vya mapato. Aidha, Shirika limepanga kutumia jumla ya TSH 12,394,854,836 kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo. Ikiwa TSH 9,465,428,856 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, TSH 2,007,295,980 ni mshahara na TSH 922,130,000 kwa kazi za maendeleo.

## D.3. MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI

108. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar ina jukumu la kusimamia, kudhibiti na kuendeleza Usafiri wa Baharini. Miongoni mwa kazi zake ni kusimamia usalama na ulinzi wa vyombo vya baharini pamoja na uhifadhi wa mazingira ya baharini, kusimamia shughuli za ukaguzi na usajili wa meli, utoaji wa leseni za makampuni yanayojishughulisha na huduma za bandarini, utoaji wa leseni kwa vyombo vidogo vidogo, utoaji wa leseni za manahodha na wahandisi wa vyombo vidogo vidogo, utoaji wa hati na vitambulisho vya mabaharia pamoja na kuidhinisha (endorsement) vyeti vya mabaharia. Aidha, Mamlaka ina jukumu la kudhibiti safari za vyombo vya baharini, uchunguzi wa ajali za baharini, uratibu wa shughuli za utafutaji na uokozi kwa ajali za baharini pamoja na usimamizi wa maslahi, ustawi na malalamiko ya mabaharia.

109. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Mamlaka ya Usafiri Baharini imefanikiwa kutekeleza yafuatayo: -

a. **Usajili wa Meli za Kimataifa na Meli za Ndani.** Kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Mamlaka

ilikadiria kusajili jumla ya meli **162** na hadi kufikia mwezi wa Machi, 2023 meli 230 zilisajiliwa zenye 'gross tonnage' (GT) 952,074 sawa na asilimia 142 ya ya meli zilizopangwa kusajiliwa katika kipindi hicho. Kati ya meli hizo, meli 228 ni usajili wa meli za kimataifa zenye GT 950,723 na meli 2 ni usajili wa ndani zenye GT 1,351.

**b. Usajili wa Vyombo Vidogo Vidogo.** Mamlaka Usafiri Baharini ilipanga kusajili jumla ya vyombo vidogo vidogo 495 kwa kipindi cha miezi tisa na hadi kufikia Machi, 2023 jumla ya vyombo vidogo vidogo 800 vilisajiliwa sawa na asilimia 162 ya makadirio ya kipindi hicho.

**c. Vitabu vya Ubaharia (Discharge Book).** Kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Mamlaka ilipanga kutoa vitabu 525 vya ubaharia na hadi kufikia Machi, 2023 imefanikiwa kutoa vitabu 746 sawa na asilimia 142 ya makadirio ya kipindi hicho.

**d. Vyeti na Mikataba ya Mabaharia Wanaosafiri Nje ya Nchi.** Kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi 2023, Mamlaka ilikadiria kuthibitisha vyeti 45 vya mabaharia wanaosafiri nje ya nchi na hadi kufikia Machi, 2023 imefanikiwa kuthibitisha vyeti 124 sawa na asilimia 275 ya makadirio ya kipindi hicho. Vile vile Mamlaka ilikadiria kuthibitisha mikataba 155 kwa mabaharia wanaosafiri na meli za nje kupitia kampuni ya DANAOS. Hadi kufikia Machi 2023 jumla mikataba 177 imethibitishwa sawa na asilimia 114 ya makadirio ya kipindi hicho.

**e. Kuthibitisha Vyeti vya Mabaharia wa Kigeni.** Mamlaka ilikadiria kuthibitisha vyeti vya mabaharia wa kigeni 360 na hadi kufikia Machi, 2023 jumla ya vyeti 265 vilithibitishwa sawa na asilimia 74 ya makadirio ya kipindi cha robo tatu.

**f. Kutoa Leseni Zinazohusu Huduma za Usafiri wa Baharini.** Mamlaka ya Usafiri Baharini ilipanga kutoa leseni 110 kwa Taasisi zinazotoa huduma za usafiri baharini kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023. Hadi kufikia Machi, 2023 jumla ya leseni 118 zimetolewa sawa na asilimia 107 ya makadirio ya kipindi hicho. Kati ya leseni hizo, leseni 58 zimetolewa kwa Mawakala wa utoaji wa mizigo bandarini, leseni 4 kwa ajili "Jetty Installation", leseni 15 kwa vituo vya uzamiaji baharini, leseni 3 kwa vyombo vya starehe, leseni 5 kwa vyombo vya michezo baharini, leseni 4 kwa kampuni zinazomiliki meli moja, leseni 3 kwa kampuni zinazomiliki meli zaidi ya moja, leseni 2 kwa mawakala wa meli za kigeni, leseni 3 kwa kampuni za michezo ya vishada baharini, leseni 13 kwa ajili ya mawakala wauza tiketi, leseni 1 kwa kampuni inayotoa mafunzo ya uzamiaji baharini, leseni 1 kwa ukaguzi wa vifaa vya uzamiaji baharini, leseni 1 kwa kampuni ya ukaguzi wa vifaa vya kuokolea maisha melini, leseni 1 kwa wafungaji wa mizigo ya melini na leseni 4 kwa hoteli zinazoelea baharini.

**g. Ukaguzi wa Meli.** Kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Mamlaka Usafiri Baharini ilipanga kukagua meli 64 na hadi Machi, 2023 imefanikiwa kukaguwa jumla ya meli 45 za ndani zenye GT 55,305 sawa na asilimia 70 ya makadirio ya miezi tisa. Kati ya meli hizo, meli 23 zenye jumla ya GT 24,599 zilifanyiwa ukaguzi wa kiusalama wa mwaka, meli 7 zenye GT 12,527 zilifanyiwa ukaguzi wa dharura, meli 1 yenye GT 19,630 ilifanyiwa ukaguzi wa chini ya maji, na meli 14 zenye GT 16,289 zilifanyiwa ukaguzi wa chelezoni.

**h. Mfumo wa Kusajili Meli na Mabaharia.** Kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Mamlaka ya Usafiri Baharini imefanikiwa kufunga vifaa vya mfumo wa kielektroniki

wa usajili wa meli na mabaharia ikiwa ni sehemu ya makubaliano ya mkataba baina ya Mamlaka na kampuni ya 'Ocean HQ Company Ltd' ya Uingereza. Aidha, Mamlaka kwa sasa inafaidika na matumizi ya mfumo huo hasa kwa usajili wa meli za Kimataifa kwa kutoa huduma zilizo bora na zenye kukidhi hadhi ya Kimataifa na kuongeza udhibiti katika ukusanyaji wa mapato.

i. **Kuimarisha Mfumo wa Ufuatiliaji Nyenendo za Meli na Vyombo Vidogo Vidogo Vilivyopo Baharini.** Kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Mamlaka ya Usafiri Baharini imefanikiwa kununua vifaa mbali mbali vya kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji wa nyenendo za meli na vyombo vidogo vidogo baharini kwa kuzifanyia matengenezo antenna zilizofungwa katika minara ya Makunduchi, Chumbe, Nungwi na Kigomasha pamoja na kuweka vifaa vipya ikiwemo solar battery 8 na inverter 4. Vilevile, Mamlaka imetenga sehemu maalum kwa ajili ya Usimamizi na utumiaji wa mfumo huo.

j. **Kufanya Marekebisho ya Sheria na Kuiandika Upya.** Mamlaka ya Usafiri Bahari ikishirikiana na Wizara inaendelea kuifanyia marekebisho Sheria ya Usafiri Baharini (namba 5 ya mwaka 2006) na hatua iliyofikiwa kwa sasa ni kuiwasilisha katika kikoa cha Baraza la Mapinduzi kwa kujadiliwa na hatimae kuwasilishwa Baraza la Wawakilishi.

k. **Kuwajengea Uwezo Wafanyakazi wa Mamlaka:** kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Mamlaka imeweza kuwajengea uwezo wafanyakazi 31 kwa kuwapatia mafunzo katika fani mbali mbali ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Kati ya hao, wafanyakazi 13 walipatiwa mafunzo maalum ya ukaguzi wa meli ambayo yaliendeshwa

hapa Zanzibar na Mtaalum kutoka Kampuni ya Maritime Bureau of Africa. Vile vile, wafanyakazi 7 walipatiwa mafunzo ya muda mrefu na wafanyakazi 11 walipatiwa mafunzo ya muda mfupi.

l. **Kuupitia Mpango Mkakati wa Mamlaka.** Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Mamlaka ya Udafiri Baharini imefanikiwa kuufanyia mapitio Mpango Mkakati wa Taasisi hiyo na kutayarisha mpango mkakati mpya wa 2023/2028 na utaanza kutumika katika mwaka wa fedha 2023/2024.

m. **Kusimamia Suala la Uuzaji wa Tiketi za Meli / Boti za Abiria.** Mamlaka ya Usafiri Baharini katika kulisimamia suala la uuzaji wa tiketi za meli na Meli za abiria inaendelea kuwaelimisha wananchi kupitia vyombo vya habari kama vile ZBC redio na TV, redio Jamii ya Micheweni na Mkoani, Wasafi TV, Bahari FM, Pemba Cable na gazeti la Zanzibar Leo kwa kutoa matangazo 169 yanaowaelimisha wananchi umuhimu wa kukata tiketi kwa kutumia kitambulisho wakati wanaposafiri. Vile vile, katika kupambana na vitendo vya ulanguzi wa tiketi, Mamlaka imewakamata watu 7 wanaojihusisha na vitendo vya ulanguzi. Kati ya hao 6 walitozwa faini na mmoja (1) kesi yake ipo kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria. Aidha, katika kipindi cha miezi tisa, abiria 501 wamezuiliwa kusafiri baada ya tiketi zao za kusafiria kuonekana taarifa zao hazifanani na taarifa zilizomo katika vitambulisho vyao.

**Mapato na Matumizi**

110. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Usafiri Baharini kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilikadiria kukusanya jumla ya TSH 6,257,812,065 kupitia vyanzo vyake vya mapato. Kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Mamlaka ilikadiria

kukusanya jumla ya TSH 4,693,359,049 na hadi kufikia Machi, 2023, jumla ya TSH 3,718,109,056 zimekusanywa sawa na asilimia 79 ya makadirio ya robo tatu na asilimia 59 kwa makadirio ya mwaka.

Kwa upande wa matumizi, Mamlaka ya Usafiri Baharini kwa mwaka wa fedha 2022/2023, ilikadiria kutumia jumla ya TSH 6,182,871,420 kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2023, jumla ya TSH 2,835,570,651 zimetumika sawa na asilimia 46 kwa makadirio ya bajeti kwa mwaka. Kati ya fedha hizo, TSH 1,049,340,487 ni mshahara na TSH 1,786,230,164 ni kwa matumizi mengineyo.

## MALENGO YA MAMLAKA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**111. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Usafiri Baharini kwa mwaka wa fedha 2023/2024 imepanga kusajili Meli 308 za ndani na kimataifa, kutoa leseni 1,200 kwa vyombo vidogo vidogo, kutoa leseni 840 za Manahodha, kutoa vitabu 1,080 vya Mabaharia (Discharge Books), kuidhinisha mikataba 300 ya Mabaharia na vyeti 160 vya mafunzo ya ulinzi melini (Maritime Security awareness) kwa Mabaharia wanaosafiri na meli za nje kupitia kampuni ya DANAOS pamoja na kuthibitisha vyeti 580 vya Mabaharia wa kigeni (Endorsements).

Vile vile, Mamlaka imepanga kutoa Leseni 286 zinazohusu huduma za Usafiri wa Baharini, kufanya Ukaguzi wa Meli 70, Kuwajengea uwezo wafanyakazi 33 pamoja na kutayarisha Kanuni 5 na miongozo 20 (Standard Operation Procedures - SOP) ya kufanyia kazi.

**Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2023/2024**

**112. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Mamlaka ya Usafiri Baharini imekadiria kukusanya jumla ya TSH 6,483,983,836 na imepanga kutumia jumla ya TSH 6,409,515,120 kwa matumizi ya kazi za kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo, jumla ya TSH 2,190,172,920 ni mshahara, TSH 4,019,342,200 kwa matumizi mengineyo na TSH 200,000,000 kwa kazi za maendeleo.

## D.4. MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR

**113. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ina jukumu la kuviendesha, kuvisimamia, na kuvitunza viwanja vya ndege vya Serikali pamoja na kusimamia usalama wa safari za abiria, ndege na mizigo katika viwanja vya ndege vya Serikali. Aidha, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege wakati wa utekelezaji wa majukumu yake inazingatia taratibu na sheria zote za uendeshaji wa viwanja kama zinavyoelekezwa na Tanzania Civil Aviation Authority (TCAA) na International Civil Aviation Organization (ICAO).

**114. Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imefanikiwa kutekeleza yafuatayo: -

**a. Kuhudumia safari za Ndege, Abiria na Mizigo**

**115. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Viwanja vya Ndege inaendelea kutekeleza kazi zake za kawaida za kuhudumia safari za ndege, abiria na mizigo katika viwanja vya Ndege Unguja na Pemba. Kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, jumla ya safari za ndege 48,718 zimehudumiwa sawa na asilimia 79 ya makadirio ya safari 61,974 zilizopangwa kuhudumiwa katika kipindi hicho. Kati ya safari hizo, safari za ndege 44,656 zilihudumiwa katika Uwanja wa Ndege

wa Kimataifa wa Abedi Amani Karume na safari za ndege 4,062 zilihudumiwa katika Uwanja wa Ndege wa Pemba. Safari za ndege za Kimataifa zilikuwa ni 9,987 na safari za ndani zilikuwa ni 38,731 **Kiambatanisho nambari 12 A** kinahusika.

**116. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka kwa mwaka wa fedha 2022/2023, imehudumia jumla ya Mashirika na Kampuni za ndege 44 za ndani na nje katika Viwanja vya Ndege vya Zanzibar. **Kiambatanisho nambari 12B** kinahusika.

Aidha, jumla ya abiria 1,573,571 wamehudumiwa sawa na asilimia 118 ya makadirio ya abiria 1,337,126 waliopangwa kuhudumiwa kwa kipindi cha miezi tisa, kati ya hao, Abiria, 1,500,041 walihudumiwa katika Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Abedi Amani Karume na abiria 73,530 walihudumiwa katika Uwanja wa ndege wa Pemba. Kati ya abiria hao, abiria 947,557 wakiwa ni wa safari za kimataifa na abiria 626,014 ni wa safari za ndani. Jumla ya Abiria waliopita (transit passengers) ni 321,201 ambapo 321,083 walipita katika Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Abedi Amani Karume na abiria 118 walipita katika Uwanja wa ndege wa Pemba. **Kiambatanisho nambari 13 C** kinahusika.

Kwa upande wa mizigo, jumla tani 1,887 zilihudumiwa katika Uwanja wa Ndege Kimataifa wa Abeid Amani Karume sawa na asilimia 74 ya tani 2,558 zilizokadiriwa kwa kipindi hicho.

### b. Kuimarisha Ulinzi na Usalama wa Viwanja vya Ndege Unguja na Pemba

**117. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha ulinzi na usalama wa Viwanja vya Ndege, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imewapatia wafanyakazi 23 mafunzo ya "basic STP

123 Aviation Security", wafanyakazi 5 mafunzo ya "Quality Management System" (QMS) na wafanyakazi 8 mafunzo ya "Security Supervisor Course" ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi na uweledi zaidi. Aidha Mamlaka imevifanyia matengenezo ya kawaida vifaa 21 vya ulinzi na usalama ikiwemo milango ya ukaguzi pamoja na mashine za ukaguzi katika Uwanja wa AAKIA na Pemba pamoja kujenga uzio wa zege wenye urefu wa kilomita moja katika uwanja wa AAKIA ili kuzuia wanyama kuingia katika maeneo ya ndani ya kiwanja.

**c. Uwekaji wa Taa za Kuongozea Ndege (Precission Lights)**

**118. Mheshimiwa Spika,** Wizara ikishirikiana na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imefanikiwa kukamilisha taratibu za manunuzi kwa ajili ya uwekaji wa taa za kuongozea ndege (Precission Lights) zitakazofanya kazi sambamba na mfumo wa kumuongoza Rubani (Instrument Landing System). Kazi hiyo itatekelezwa na Kampuni ya MS ADB SAFE GATE na kazi za ujenzi zilitarajiwa kuanza mwezi Machi 2023 na kukamilika Machi, 2024 kwa gharama ya USD 70,773.17. Mradi huu utakapokamilika utamuwezesha Rubani kutua katika uwanja wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume kwa usalama zaidi hasa nyakati za usiku pamoja na hali mbaya ya hewa.

**d. Uimarishaji wa Miundombinu ya Viwanja vya Ndege Unguja na Pemba**

**119. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha miundombinu ya Viwanja vya Ndege Unguja na Pemba, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imefanikiwa kufanya ukarabati jengo la abiria Nambari 2 linalotumika sasa katika Uwanja wa AAKIA kwa kujenga njia ya kupita abiria "Walk Way" kutoka jengo la abiria

Nambari 2 hadi jengo la abiria Nambari 3, Ujenzi wa eneo jipya la kuondokea abiria wa ndani, Ujenzi wa njia “Walk Way“ katika eneo la kuondokea abiria wa ndani pamoja na njia ya kupita abiria kuelekea katika ndege, Ujenzi wa eneo la ukaguzi wa wafanyakazi na vyombo vinavyoingia (Cargo), Ujenzi wa mtaro wa maji ya mvua kutoka mbele ya jengo la kuongozea ndege, Ununuzi wa jenereta la akiba la 1,250KVA pamoja na kulifanyia matengenezo jengo la abiria la Uwanja wa ndege wa Pemba kwa kufanya utanuzi wa eneo la kuwasili abiria.

**e. Uimarishaji wa Mazingira ya Biashara Katika Uwanja wa Ndege wa AAKIA**

**120. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka imefanikiwa kuimarisha mazingira ya biashara katika Uwanja wa AAKIA kwa kuingia Mkataba na Kampuni ya Emirates Leisure kutoka UAE kwa ajili ya kuimarisha na kuendesha huduma za maduka na migahawa kwa hadhi ya kimataifa katika Jengo la tatu la abiria. Kampuni hiyo inatoa huduma za vinywaji na chakula, maduka yanayojumuisha bidhaaa mbali mbali zikiwemo za kiasili pamoja na kumbi za wageni. Aidha, Mamlaka imeingia makubaliano na kampuni ya DNATA kwa ajili ya uendeshaji wa kumbi za wageni mashuhuri na wafanyabiashara mashuhuri (VIP na CIP) pamoja na utoaji wa huduma za ndege na mizigo (ground handling services). Kampuni zote hizo tayari zinaendelea kutoa huduma mbalimbali katika Uwanja wa AAKIA kama mikataba yao inavyoelekeza. Kwa sasa huduma za biashara pamoja na huduma za ndege (Ground Handling Services) katika Jengo la abiria TerminaL 3 zimeimarika na zinatolewa kwa viwango vya kimataifa.

**f. Matengenezo ya Njia ya Kupitia ndege "Taxiway C" Katika Uwanja wa AAKIA**

**121. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ilipanga kuifanyia matengenezo njia ya kupitia ndege "Taxiway C" katika Uwanja wa Ndege wa AAKIA. Kazi hii itafanywa na kampuni ya OCKRA(Z) CONSTRUCTION kwa gharama ya TSH 815,059,800 na ilitarajiwa kuanza mwezi Aprili 2023 na kumalizika mwezi Aprili 2024. Mkandarasi kwa sasa anaendelea na maandalizi ya kuleta vifaa kwa ajili ya kuanza kazi.

**g. Upembuzi Yakinifu kwa Ajili ya Ujenzi wa jengo la Abiria (Terminal 4)**

**122. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imeanza maandalizi ya Ujenzi wa Jengo jipya la nne la abiria (Terminal 4) katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume ambapo kwa sasa ripoti ya awali ya Upembuzi yakinifu na michoro ya kina kwa ajili ya ujenzi wa jengo hilo la abiria imewasilishwa

**h. Uondoshaji wa Mabaki (Friction) ya Mipira ya Ndege Zinazotua na Kuruka Katika Uwanja wa Ndege wa AKIAA**

**123. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ilipanga kuondosha mabaki ya mipira ya ndege zinazotua na kuruka katika barabara ya kurukia na kutulia ndege katika Uwanja wa ndege wa AAKIA. Kazi hiyo imekamilika na imefanywa na kampuni ya Road Grip kwa gharama ya TSH 521,245,420.

**Mapato na Matumizi**

**124. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar ilikadiria

kukusanya jumla ya TSH 34,000,520,866 na kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 ilikadiria kukusanya jumla ya TSH 26,624,338,342 kupitia vyanzo vyake vya ndani. Hadi kufikia Machi, 2023, jumla ya TSH 23,747,900,013 zimekusanywa sawa na asilimia 89 ya makadirio ya robo tatu na asilimia 70 ya makadirio ya mwaka.

**125. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa matumizi, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar ilipanga kutumia jumla ya TSH 31,084,201,869 kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo. Kati ya fedha hizo, TSH 11,471,894,469 ni kwa matumizi mengineyo, TSH 9,684,068,400 ni mshahara na TSH 9,928,239,000 kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2023, jumla ya TSH 19,719,112,027 zimetumika sawa na asilimia 68 ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo TSH 4,343,255,284 ni mshahara, TSH 11,339,370,447 ni matumizi mengineyo na TSH 4,036,486,296 ni kwa kazi za maendeleo.

## MALENGO YA MAMLAKA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**126. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imepanga kuendelea kuimarisha ulinzi na usalama ili kukidhi viwango vya Kitaifa na Kimataifa kwa kuwapatia wafanyakazi mafunzo ya ulinzi na usalama katika fani mbalimbali. Aidha, Mamlaka imepanga kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa jengo jipya la abiria (Terminal 4), utanuzi wa jengo la abiria, Ujenzi wa kituo cha biashara (business center) katika jengo la Terminal 3, Ukarabati wa kumbi za wageni mashuhuri katika jengo la abiria la Terminal 1 na Terminal 2, Kuimarisha huduma za zimamoto na uokozi Unguja na Pemba, kuimarisha huduma katika majengo ya Abiria Unguja na Pemba pamoja na kuwapatia mafunzo ya uendeshaji na usimamizi wa Uwanja wafanyakazi wa Mamlaka Pemba. Aidha, Mamlaka

imepanga kuhudumia abiria 1,896,316, Ndege 76,370 na Mzigo tani 3,406 kwa Unguja na Pemba.

**Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2023/2024**

**127. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imekadiria kukusanya jumla ya TSH 42,183,292,873 kupitia vyanzo vyake vya mapato na imepanga kutumia jumla ya TSH 38,897,172,670. Kati ya hizo, TSH 21,940,426,270 kwa kazi za kawaida na TSH 16,956,746,400 kwa kazi za maendeleo.

## D.5 MAMLAKA YA USAFIRI NA USALAMA BARABARANI

**128. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani imepewa jukumu la kusimamia usafiri barabarani kwa kudhibiti usalama wa watumiaji wa barabara, utoaji wa huduma za usafiri barabarani pamoja na kusimamia Kamati ya Kitaifa ya Usalama Barabarani.

**Malengo ya Mamlaka kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

**129. Mshehimiwa spika,** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Zanzibar itaendelea kutoa huduma za usafiri barabarani ikiwemo utoaji wa leseni 22,315 za madereva wanafunzi, Kuwafanyia majaribio ya udereva madereva 10,643, Kutoa vibali 27,249 kwa madereva wageni, Kutoa leseni 14,209 kwa vyombo vya Biashara, Kutoa ruhusa za njia za usafirishaji 17,853 pamoja na Kutoa beji za madereva na utingo 11,432. Vilevile, Mamlaka itaendelea kuimarisha usalalama wa watumiaji wa barabara kwa kuwapatia elimu ya usalama barabarani pamoja na Kuvifanyia ukaguzi vyombo vya moto 67,547 vya Serikali na Binafsi.

Aidha, Mamlaka imepanga kuanzisha mfumo wa udhibiti wa usalama barabarani (Traffic Managemnt System) ambao utahusisha uandaaji wa mfumo wa usajili wa vyombo utakaoendana na mifumo ya Mamlaka ikiwemo mfumo wa vifaa vya kufuatilia vyombo vya moto (Vehicles Tracking System) na mfumo wa "Taxi" mtandao.

Pia, Mamlaka imepanga kuanzisha kituo kimoja cha huduma za usafiri barabarani ambacho kitahusisha kituo cha kisasa cha ukaguzi wa vyombo vya moto vilivyopo nchini pamoja na kumalizia mfumo wa uombaji wa leseni ya udereva kwa njia ya mtandao (ZODLAP II).

**Makadirio ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024**

130. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kwa mwaka wa fedha 2023/2024 imekadiria kukusanya jumla ya TSH 4,387,679,000 kupitia vyanzo vyake vya mapato na imepanga kutumia jumla ya TSH 3,385,266,276 kwa kazi za kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo, TSH 1,251,895,276 ni matumizi mengineyo, TSH 1,259,571,000 ni mshahara na TSH 873,800,000 kwa kazi za maendeleo.

## D.6 WAKALA WA MIUNDOMBINU YA TEHAMA

**Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA (ZICTIA) imepewa jukumu la kusimamia na kuendesha Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano wa Zanzibar, kusimamia kituo kikuu cha kuhifadhia taarifa (Data Center) cha Serikali pamoja na Minara ya mawasiliano ya simu.

**Malengo ya ZICTIA kwa Mwaka wa fedha 2023/2024**

131. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA kwa mwaka wa fedha 2023/2024 imepanga kuimarisha

huduma za Mkonga, Data Center pamoja na minara Unguja na Pemba. Pia, ZICTIA imepanga kuanzisha huduma mpya za kutumia Kamera za Mji Salama, Kuongeza wigo wa upatikanaji wa "Public WiFi" katika maeneo yenye mikusanyiko ya shughuli za kiuchumi na kijamii Unguja na Pemba pamoja na kuufikisha Mkonga wa mawasiliano katika majengo yote ya biashara na makaazi (Fiber to the home technology). Aidha, ZICTIA imepanga kuanza rasmi Ujenzi wa Kituo Mbadala cha Kuhifadhia Taarifa (Data Recovery Site) katika Maeneo ya uwekezaji Fumba pamoja na kulaza mkonga wa kimataifa (International Gateway) kutoka Mombasa Kenya.

132. **Mheshimiwa Spika,** Kutokana na ujenzi wa miundombinu ya barabara mbali inayoendelea Unguja na Pemba, Wizara kupitia ZICTIA imepanga kuhamisha na kutengeneza Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano ili kupisha shughuli za ujenzi wa miradi hiyo. Pia, ZICTIA imepanga kuendelea na kazi ya kuviunganisha na mkonga vituo vya taasisi mbali ambavyo havijaunganishwa ili kuimarisha huduma za Serikali.

133. **Mheshimiwa Spika,** Pia, ZICTIA kwa mwaka wa fedha 2023/2024 imepanga kuimarisha njia ya kusafirishia mawasiliano kupitia Minara (Microwave Transmission System), kutoka Nungwi kwa upande wa Unguja hadi Kichunjuu kwa upande wa Pemba. Vilevile, ZICTIA imepanga kuanza rasmi kutoza malipo kwa taasisi zote za Serikali zinazotumia huduma za mtandao.

**Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

134. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wakala wa Miundombinu TEHAMA Zanzibar limekadiria kukusanya jumla ya TSH. 7,000,000,000 kutoka katika

vyanzo vyake vya mapato na imepanga kuchukua mkopo wa jumla ya TSH 16,050,800,000 ikiwa ni mtaji kwa ajili ya kuanzisha Shirika la Mawasiliano Zanzibar. Na imepanga kutumia jumla ya TSH15,403,688,500,000 kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo. Ikiwa TSH 1,227,141,780 ni Mshahara, TSH 4,306,246,720 ni kwa matumizi mengineyo na TSH 9,870,300,000 ni kwa kazi za maendeleo.

## E. MUELEKEO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI KWA KILA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

135. **Mheshimiwa Spika,** baada ya kutoa maelezo ya utekelezaji kwa kila programu zinazosimamiwa na Wizara kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, pamoja na kutoa maelezo ya Utekelezaji kwa kipindi cha miezi tisa (Julai - Machi 2023) na Malengo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kwa Taasisi zinazojitegemea zilizo chini ya Wizara, sasa naomba kuwasilisha muelekeo wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

## E.1. VIPAUMBELE VIKUU VYA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

136. **Mheshimiwa Spika,** Matayarisho ya bajeti hii yamezingatia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar (2050), Sera ya Taifa ya Usafiri Zanzibar (2008), Mpango Mkuu wa Usafiri Zanzibar (Zanzibar Transport Master Plan - 2007), Mpango wa Taifa wa Maendeleo Zanzibar - ZADEP (2021- 2026), Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (2013), Sera mbalimbali za sekta mtambuka za Taifa, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2020-2025), Matokeo ya Sensa ya Watu na Makaazi ya mwaka 2022, ahadi pamoja na maagizo mbalimbali yaliyotolewa na Viongozi Wakuu wa Serikali. Pia, Bajeti hii imezingatia vipaumbele vikuu vya Serikali

kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ikiwemo kuimarisha miundombinu ya bandari, miundombinu ya usafiri wa barabara, miundombinu ya usafiri wa Anga pamoja na miundombinu ya mawasiliano.

## E.2 MUHTASARI WA MAELEZO KWA KILA PROGRAMU NA MALENGO YANAYOTARAJIWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

137. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia Sekta ya Usafirishaji na Mawasiliano kupitia Programu Kuu tatu (3) ambazo ni; - Programu ya Usafirishaji, Programu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) pamoja na Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi.

138. **Mheshimiwa Spika,** programu kuu zilizoainishwa katika bajeti hii zimewekewa malengo makhususi, matokeo ya muda mrefu yatakayopatikana, huduma zitakazotolewa, shabaha na viashiria mbalimbali vitakavyotumika kupima utekelezaji wa huduma zitakazotolewa katika Sekta ya Mawasiliano na Sekta ya Usafirishaji. Maelezo ya programu hizo ni kama ifuatavyo:

### E.2.1 PROGRAMU YA USAFIRISHAJI.

139. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ina lengo la kuwepo kwa miundombinu bora na huduma za usafiri zilizo bora, salama na endelevu. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu ya Usafirishaji itakuwa na programu ndogo moja ambayo ni; Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji.

### E.2.1.1 Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji

**140. Mheshimiwa Spika,** programu hii ndogo inasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Wakala wa Barabara Zanzibar pamoja na Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar. Programu hii ina lengo la kuhakikisha huduma bora za usafiri zilizo salama zinapatikana muda wote Unguja na Pemba. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara kupitia Taasisi zinazozimamamia programu hii, imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

### 1. IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

**141. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia programu ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji imepanga kuendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ifuatayo:-

a. Ujenzi wa barabara kuu nne (4) Unguja na Pemba zenye urefu wa kilomita 130.6 ambazo ni Barabara ya Wete – Chake km 22, Tunguu – Makunduchi km 53.5, Fumba – Kisauni km12 na Bara ya Chake – Mkoani km 43.

b. Ujenzi wa Barabara za ndani zenye urefu wa kilomita 275.9 Unguja na Pemba.

c. Ujenzi wa barabara za Mjini Unguja zenye urefu wa kilomita 100.9.

d. Ujenzi wa barabara kuu zenye urefu wa kilomita 277 Unguja na Pemba.

e. Uimarishaji wa Uwanja wa Ndege wa Pemba.

f. Uimarishaji wa Uwanja wa Ndege wa Nungwi pamoja na;

g. Kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa Bandari Jumuishi ya Mangapwani itakayojumuisha bandari za Mizigo, Chelezo, Mafuta na Gesi kwa kujenga miundombinu ya barabara, maji na umeme pamoja na kuendelea kutafuta wawekezaji kwa ajili ya kuekeza katika Bandari hiyo katika maeneo tofauti yaliyoanishwa katika Mpango Mkuu (Master Plan) wa ujenzi wa bandari hiyo.

**142. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imepangiwa kutumia jumla ya TSH 553,547,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo Unguja na Pemba, ikiwa TSH 324,000,000,000 ni mkopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TSH 229,547,000,000 ni mchango kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

## 2. WAKALA WA BARABARA ZANZIBAR

**143. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wakala wa Barabara Zanzibar kupitia programu ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji imepanga kuzifanyia matengenezo barabara mbalimbli Unguja na Pemba ikiwemo barabara ya Tumbatu km 9, Mbuzini maduka matano – Mwakaje km 5, Fuoni Maharibiko – Mshelishelini meli tano km 2.6, Chuwini Branch – Mawimbini km 1.6, Kilombero – Mgonjoni km 5, Kiboje – Uchukuni km 3.2, Kinyasini – Bandamaji km 2, Micheweni Msituni – Mjini Wingwi – Msasani km3.5 na Kipapo – Mgelema – Wambaa km 9.4 kwa kiwango cha lami.

Aidha, Wakala imepanga kuzifanyia matengenezo ya kawaida barabara zilizojengwa kwa lami ambazo ni Mizingani – Wambaa km 9.7, Kenya – Chambani km 3.2, Mtambile – Kangani km 6.4, Mtambile – Mwambe km 9.6 pamoja na Chanjaani – Pujini km 5. Kwa ujumla matengenezo ya Barabara hizo yanagharamiwa na Mfuko wa Barabara Zanzibar.

Kwa upande wa kazi za kawaida Wakala imepanga kuendelea kutekeleza shughuli za kiutumishi na utawala kwa kununua vifaa mbalimbali vya Ofisi pamoja na kulifanyia matengenezo jengo la Ofisi kuu lililopo Saateni. Pia, Wakala imepanga kuwapatia mafunzo ya muda mfupi Wafanyakazi 15 na mafunzo ya muda mrefu Mfanyakazi mmoja

**144. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wakala wa Barabara Zanzibar imepangiwa kutumia jumla ya TSH 13,718,700,000 kutoka Mfuko wa Barabara kwa ajili ya mtengenezo ya Barabara Unguja na Pemba.

**145. Mheshimiwa Spika,** Pia Wakala wa Barabara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 imepangiwa kutumia jumla ya TSH 5,216,470,000 ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, TSH 4,650,400,000 ni mshahara na TSH 566,070,000 ni matumizi mengineyo.

### 3. WAKALA WA KARAKANA KUU YA MAGARI ZANZIBAR

**146. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar kupitia Programu ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na huduma za Usafirishaji imepanga kuvifanyia matengenezo vyombo vya moto 2,080 vya Serikali na binafsi Unguja na Pemba. Pia, Wakala umepanga kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Taasisi 56 katika ununuzi na uuzaji wa gari za Serikali, kuwapatia mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi 16 katika fani za utengenezaji wa gari na Utawala. Pia Wakala umepanga kuongeza vitendea kazi na kuimarisha huduma za Ofisi na karakana zake.

**147. Mheshimiwa Spika,** ili kutekeleza malengo hayo, Wakala wa Karakana imepangiwa kutumia jumla ya TSH 1,445,230,000 ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini kwa kazi za kawaida. Kati

ya fedha hizo TSH 329,430,000 ni matumizi mengineyo na TSH 1,115,800,000 ni ruzuku ya mshahara.

148. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu na Huduma za Usafirishaji inaombewa kutumia jumla ya TSH 560,208,700,000 kwa kazi za kawaida, Ruzuku na miradi ya maendeleo kwa taasisi zinazosimamia programu hii.

## E.2.2 PROGRAMU YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA).

149. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ina lengo la kuhakikisha kuwepo kwa miundombinu na huduma bora za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) Zanzibar. Kwa mwaka wa Fedha 2023/2024 programu hii itakuwa na programu ndogo moja ambayo ni; Miundombinu na Huduma za TEHAMA.

### E.2.2.1 Programu Ndogo ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA

150. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Idara ya Mawasilino na ina lengo la kuhakikisha kuwepo kwa miundombinu na huduma bora za TEHAMA zilizo salama na endelevu. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Idara ya Mawasiliano kupitia programu hii imepanga kuendelea kusimamia huduma mbalimbli za mawasiliano kama vile posta, simu na intaneti pamoja na kutoa huduma na mafunzo ya TEHAMA kwa Wananchi wapatoa 2,500 kupitia Vituo vya TEHAMA Jamii vilivyopo katika Wilaya za Unguja na Pemba.

Pia, Idara imepanga kuweka utaratibu utakaowezesha kuwatambua, kuwaibua pamoja na kuwajengea uwezo

Wajasiriamali wanaojishughulisha na Ujasiriamali wa TEHAMA (ICT Enterprenuership) Unguja na Pemba. Katika kuimarisha huduma za mawasiliano, Idara ya Mawasiliano kwa kushirikiana na wadau wa Sekta ya Mawasilano itaweka miundombinu katika maeneo yote yaliyobainika kuwa na changamoto ya mawasiliano ili kuwezesha kupatikana wa huduma za sauti na data katika maeneo hayo.

Aidha, Wizara kupitia Idara ya Mawasiliano itaendelea kutekeleza mfumo wa Anuani za Makaazi kwa kuweka Miundombinu wezeshi katika maeneo yote Unguja na Pemba, kuendelea kufanya uhakiki wa anuani zilizopo pamoja na kutoa anuani mpya katika maeneo yote yatakayojengwa miundombinu mipya ya barabara na majengo.

**151. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Programu Ndogo ya Miundombinu na Huduma za TEHAMA inaombewa kutumia jumla ya TSH 6,599,771,000 kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo. Kati ya fedha hizo, TSH 400,700,000 ni matumizi mengineyo, TSH 299,071,000 ni mshahara na TSH 5,900,000,000 kwa ajili ya kazi za maendeleo.

### E.2.3 PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA.

**152. Mheshimiwa Spika,** programu hii ina lengo la kuhakikisha kuwa Wizara inaratibu na kutayarisha Sera na Mipango bora katika Sekta ya Mawasiliano na Usafirishaji pamoja na usimamizi mzuri wa rasilimali watu. Programu hii ina programu ndogo tatu (3) ambazo ni; Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji, Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara pamoja na Uratibu wa shughuli za Wizara Pemba.

### E.2.3.1. Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji

**153. Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi na ina lengo la kuimarisha huduma za ofisi na usimamizi wa rasilimali watu katika Wizara.

**154. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Idara ya Uendeshaji na Utumishi kupitia programu hii itaendelea kutekeleza masuala ya kiutumishi na Uendeshaji wa Wizara ikiwemo kuweka mazingira mazuri ya kazi, kusimamia maslahi ya watumishi, kununua vitendea kazi ili kuongeza ufanisi wa kazi. Aidha, Idara ya Uendeshaji na Utumishi itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kuratibu maelekezo na miongozo yote kuhusiana na masuala ya kiutumishi kama yatakavyotolewa. Vilevile, Idara imepanga kutoa Makala na machapisho mbalimbali kuhusu utekelezaji wa shughuli na mafanikio ya Wizara.

**155. Mheshimiwa Spika,** ili kuongezea ujuzi, ufanisi na tija kwa wafanyakazi wa Wizara, Idara imepanga kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi wafanyakazi 41 wa Wizara Unguja na Pemba kwa mujibu wa mpango wa mafunzo wa Wizara.

**156. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Programu ndogo ya Usimamizi wa Utawala na Uendeshaji inaombewa kutumia jumla ya TSH 2,760,140,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, TSH 1,610,140,000 ni mshahara na TSH 1,150,000,000 ni kwa matumizi mengineyo.

### E.2.3.2 Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara

**157. Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na ina lengo la kuhakikisha Mipango na Sera mbalimbali za Sekta ya Mawasiliano na Usafirishaji zinatayarishwa pamoja na kufuatilia utekelezaji wake.

**158. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia programu hii imepanga kuendelea kuratibu na kufuatilia upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kufanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Wizara, kutayarisha muongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya utekelezaji wa kazi za Wizara, kutoa mafunzo ya utayarishaji wa bajeti kwa watendaji wa Wizara kulingana na miongozo kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, kuratibu na kufanya tafiti zinazohusu sekta ya Usafirishaji na Mawasiliano, kufanya mapitio Sera ya Taifa ya Usafiri ya mwaka 2008 na Sera ya TEHAMA ya mwaka 2013. Pia, Idara itaendelea kukusanya na kuchambua takwimu za maendeleo ya sekta na kuweka mpango bora wa utunzaji wa kumbukumbu za takwimu.

**159. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imepanga kuratibu mapitio Sheria na Kanuni zinazosimamia sekta ya Usafiri na Mawasiliano kwa kuzifanyia marekebisho ili ziendane sambamba na mahitaji na mabadiliko yaliopo kwa sasa. Pia, Idara itaendelea kuratibu mashirikiano ya kisekta baina ya Taasisi za ndani na nje ya nchi kikanda na Kimataifa ikiwemo vikao vya mashirikiano baina ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi (SMZ), Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (SMT) pamoja na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (SMT). Vilevile, Idara itaendelea kuratibu Taasisi na Mashirika yanayojitegemea yaliyochini Wizara.

**160. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara inaombewa kutumia jumla ya TSH 922,308,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizio, TSH 342,308,000 ni mshahara na TSH 580,000,000 ni matumizi mengineyo.

#### E.2.3.3 Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba

**161. Mheshimiwa Spika,** programu hii inasimamiwa na Ofisi Kuu Pemba na ina lengo la kuhakikisha majukumu ya Wizara yanatekelezwa ipasavyo kwa upande wa Pemba.

**162. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Ofisi Kuu Pemba imepanga kutekeleza kazi zake kama ifuatavyo; kuratibu na kusimamia maslahi ya wafanyakazi, kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi wafanyakazi 11, kutoa huduma mbali mbali za kuendeshea Ofisi, kutoa mafunzo ya mtambuka, kutoa mafunzo TEHAMA jamii kwa wananchi wa Wilaya zote za Pemba, kuendelea na uratibu wa anuani za makaazi na Postcode, kuratibu na kusimamia miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa upande wa Pemba ikiwemo kufanya malipo ya fidia kwa miradi mbali mbali itakayotekelezwa pamoja na kusimamia utekelezaji wa mipango na bajeti ya Wizara. Pia Ofisi Kuu Pemba imepanga kulifanyia matengenezo jengo la Ofisi liliopo Chake Chake Pemba. Kwa ujumla, malengo yote yanayosimamiwa na Idara husika, Ofisi Kuu Pemba inaratibu malengo hayo kwa kila Idara kwa upande wa Pemba.

**163. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Programu Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba inaombewa kutumia jumla ya TSH 999,781,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, TSH 499,781,000 ni mshahara na TSH 500,000,000 ni kwa matumizi mengineyo.

## F. HITIMISHO

**164. Mheshimiwa Spika,** kabla sijamaliza hotuba yangu hii sina budi kutoa shukurani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu na ustahamilivu wakati wote nilipokua nikitoa maelezo ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi. Ni matumaini yangu kwamba Baraza lako Tukufu litatoa michango ambayo itasaidia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kuendelea kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kutatua changamoto mbalimbali ambazo zilijitokeza katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 na hatimae kuipitisha Bajeti hii kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara zilizopangwa katika kila programu kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**165. Mheshimiwa Spika,** mafanikio ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ambayo nimeyaeleza kwa kina katika hotuba hii, ni matokeo ya ushirikiano wa wadau mbalimbali wa ndani na nje ya Nchi. Kwa niaba ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, napenda kuchukua fursa hii kuzitambua, kuzishukuru na kuzipongeza Taasisi mbalimbali tulizoshirikiana nazo katika kuendeleza Sekta mbalimbali za Wizara hii. Shukurani za dhati ziende kwa Washirika wa Maendeleo wakiwemo Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Kiuchumi Afrika (BADEA), Saudi Fund, UK Export Finance ya Uingereza na Mashirika ya Umoja wa Mataifa yakiwemo IMO na ICAO.

**166. Mheshimiwa Spika,** vile vile, natoa shukurani zangu kwa Taasisi binafsi zinazotoa huduma za mawasiliano na usafirishaji hapa Zanzibar ikiwemo Kampuni za mawasiliano za TigoZantel, Halotel, Airtel, Vodacom, TTCL na Zanlink. Kwa upande wa Kampuni za usafirishaji wa baharini tunazipongeza

